BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT
1,008,534,842/-
KWA 1000/- TU!
SportPesa.CO.TZ | PIGA *150*87#



UKURASA 3

**UTATA** waibuliwa bungeni zabuni ujenzi wa SGR


ama
AFYA NA MAZINGIRA
Anenavyo Dk. Baraka Nzobo: lilivyo afya kinywa na upeo mdogo jamii kuelewa mahali penye shida
HATUA MPYA VITA UTAPIAMLO... Yabuniwa mashine mpya ya kuandaa virutubishi lishe, ishara ya mapinduzi
Namna safari ya saikolojia na falsafa inavyoangukia kwenye afya binafsi

UKURASA 11


# Nipashe

Alhamisi Juni 23, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580985

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


# Kilichowaangusha kina Mdee kortini

UKURASA 2


Esther Bulaya


Halima Mdee


Esther Matiko


Sophia Mwakagenda

# Mbunge aendeleza moto wa kikokotoo aliouwasha Bulaya

UKURASA 2



Baadhi ya abiria wa treni iliyokuwa ikitoka Kigoma kwenda Dar es Salaam wakiwa nje ya mabehewa baada ya kupata ajali eneo la Malolo mkoani Tabora jana. Abiria wanne walipoteza maisha na wengine 132 kujeruhiwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

UKURASA WA 3

## MSAKO WAHAMIAJI HARAMU LOLIONDO

KAMISHNA Jenerali wa Uhamiaji Nchini (CGI), Dk. Anna Makakala, ametangaza operesheni maalumu ya siku 10 ya kuwasaka wageni wote walioingia nchini na kuishi bila ya kufuata...

UKURASA WA 3

## WATU WANNE WALIVYOFARIKI AJALI YA TRENI

WATU wanne wakiwamo watoto wawili wamefariki dunia na wengine 132 kujeruhiwa katika ajali ya treni ya abiria iliyokuwa

UKURASA WA 4

## TEF YALAANI MGAMBO WA JIJI KUBUGUDHI WAUZAJI MAGAZETI



JUKWAA la Wahariri Tanzania (TEF) limeeleza kusikitishwa na vitendo vilivyofanywa na askari wa Jiji la Dar es Salaam vya kuwanyanyasa na kuchukua meza...

UKURASA WA 5

## MUFTI MKUU AHIMIZA CHANJO UVIKO-19

SHEIKH Mkuu wa Tanzania, Mufti Abubakar Zubeir, amewaagiza masheikh wote kuanzia ngazi za kata kuwaelimisha waumini umuhimu wa kuchanja...

## CCM: Katiba Mpya ni muhimu kwa sasa

UKURASA 2

MICHEZO SHEREHE YA KOMBE YANGA 'BABKUBWA' UK.24

MAONI, KATUNI UK.6



Kaimu Meneja wa Uwanja wa Ndege wa Bukoba, Mathar Chidodo, akimwelezea Katibu Mkuu (Sekta ya Uchukuzi), Gabriel Migire (kulia), kuhusu miundombinu ya kiwanja cha Bukoba, alipokikagua kiwanja hicho mkoani Kagera. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kilichowaangusha kina Mdee

**Na Waandishi Wetu**

MAHAKAMA Kuu Masijala Kuu imeyaondoa maombi ya waliokuwa wanachama 19 wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kwa kuwa yana upungufu mbalimbali wa kisheria.

Wabunge hao 19, wakiongozwa na Halima Mdee, walifungua maombi hayo mahakamani huko kuomba mahakama itoe kibali cha kufungua kesi ya kupinga mchakato uliowavua uanachama wa CHADEMA.

Pia waliomba mahakama iweke zuio la kutokuchukuliwa kwa hatua zozote dhidi yao hadi pale maombi yao ya msingi yatakapoamuliwa. Hadi sasa wabunge hao hawana zuio lolote kutokana na maombi hayo kutupwa.

Uamuzi mdogo huo ulitolewa jana na Jaji John Mgeta baada ya kupitia hoja za pande zote mbili na mapingamizi saba ya wajibu maombi yaliyotolewa na Wakili Peter Kibatala, ambapo yamekubaliwa mawili na matano yametupiliwa mbali.

Alisema katika maombi hayo, mawili yalikubaliwa na kwamba mahakama imeelekeza wayafanyie marekebisho.

Jaji Mgeta alisema waleta maombi (Mdee na wenzake) walikosea jina la mjibu maombi wa kwanza, walimshitaki mtu ambaye kisheria hayupo, wameishtaki Bodi ya Wadhamini ya CHADEMA badala ya wadhamini waliosajiliwa (Registered Trustee) kama sheria ilivyoelekeza.

Alisema hiyo ni kwa wa mujibu wa sheria ya vyama vya siasa kifungu cha 21(1) ambacho kinataka chama chochote cha siasa kikishapata usajili wa kudumu kiwateue na kuwasajili hao trustee kwa mujibu wa sheria ya wadhamini.

Katika mapingamizi ya Kibatala alidai kuwa wakili ana sehemu yake ya kutia saini, kitendo cha mawakili kutia saini katika viapo vya kina Mdee, kina maana wanajimilikisha maelezo ambayo ni ya kuambiwa.

Wakili Jeremia Mtobesya ambaye pia anawakilisha CHADEMA, aliiomba mahakama kutupilia mbali maombi hayo ya kina Mdee kwa kuwa wameishtaki Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ambayo haikutakiwa kushtakiwa katika shauri hilo.

Alidai NEC haikutakiwa kuunganishwa katika shauri hilo kwa kuwa mahakama haina mamlaka kisheria ya kuhoji uamuzi wake kwa mujibu wa ibara ya 74 (12) ya Katiba ya nchi.

Akijibu hoja za pingamizi hilo, Wakili Aliko Mwamanenge kwa niaba ya Halima Mdee na wenzake, aliiomba mahakama itupilie mbali mapingamizi hayo kwa sababu hoja zao hazina msingi wowote.

Alidai kuwa katika kesi hiyo, NEC bado haijataja majina au kuchagua wabunge wengine wa kujaza nafasi za kina Mdee, bali waleta maombi wanachotaka kuzuia NEC kufanya chochote.

Wakili Ebson Kilatu wa upande wa waleta maombi, akijibu hoja ya kuishitaki Bodi ya Wadhamini ya CHADEMA, alidai ni sahihi kuishitaki kwa kuwa ndicho chombo kinachofanya uamuzi wa chama.

Kuhusu hoja ya mawakili kutia saini katika viapo hivyo, Wakili Kilatu alidai hawajatia saini katika viapo hivyo, bali waliandika tarehe ya uandaaji viapo hivyo na kutia saini eneo hilo ambalo haiathiri hoja za maombi hayo.

**NJE YA MAHAKAMA**

Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, alipongeza alichokiita haki kutendeka, imeshinda udhalimu, dhuluma na usaliti, hivyo kutokana na uamuzi huo, mara moja Wakili Mkuu wa Serikali atapaswa kupeleka taarifa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na yeye ataipeleka kwa Spika wa Bunge ili kina Mdee waondolewe bungeni.

Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje, John Mrema, alisema ni tukio la kihistoria kwa CHADEMA kwa kuwa walikuwa hawajawahi kuwavua uanachama wabunge 19.

**■Imeandikwa na Grace Gurisha na Romana Mallya**

# CCM: Katiba Mpya muhimu kwa sasa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimesisitiza umuhimu wa uwapo wa Katiba Mpya kwa kuzingatia mazingira ya sasa na kuangalia namna bora ya kufufua na kukwamua mchakato wake.

Pia imeshauri serikali kuangalia namna nzuri ya kumaliza kwa haraka kesi za kisiasa zinazowakabili wanachama wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

Akizungumza jana na waandishi wa habari kuhusu vikao vya juu vya chama hicho ikiwamo cha Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (NEC), Katibu wa NEC, Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, alisema mchakato huo ukwamuliwe na kukamilika kwa maslahi ya taifa na maendeleo kwa ujumla. Aidha, alisema NEC inapongeza juhudi zote za vyama vya siasa katika kutengeneza maridhiano hayo ya kisiasa ambayo yana dhamira ya kuwaunganisha Watanzania.

"CCM inashauri serikali kuharakisha mambo yote ambayo Rais Samia alitoa dira na mwelekeo na wanasiasa wamepokea na yanakwenda vizuri," alisema.

**KESI ZA KISIASA**

Kuhusu mazungumzo kati ya CCM na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Shaka alisema mazungumzo yanakwenda vizuri na NEC imepokea taarifa ya mazungumzo hayo na imeshiriki hatua zote ili dhamira ya Rais Samia itimie.

"Tayari vikao viwili vimeshakaa upande wa CCM na CHADEMA na mazungumzo yanakwenda vizuri kwenye hayo mazungumzo tumeshauri serikali ikaangalie kesi zile za wanachama za kisiasa ambazo zipo kwenye vyombo mbalimbali vya kisheria kwa mujibu wa Katiba ya nchi, lakini kuangalia namna nzuri ya kumaliza haraka zaidi kesi hizo," alisema.

Alisema nia ni kuhakikisha malengo na azma ya maridhiano inatimia. Shaka alisema NEC imempongeza Rais Samia kwa dhamira na maono yake ya kuhakikisha milango ya maridhiano inaendelea kwa hatua kubwa ili kuhakikisha kunakuwapo na maridhiano ya kisiasa nchini.

Pia alisema NEC imempongeza Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi kwa namna anavyoleta muafaka wa kisiasa na CCM imeahidi kumpa ushirikiano ili kuleta ustawi wa amani na utulivu wa Zanzibar.

**UTEUZI**

Alisema Kamati Kuu ya CCM pamoja na mambo mengine ilifanya uteuzi wa wagombea wa nafasi ya Uenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Njombe na Halmashauri ya Ngorongoro na Manispaa ya Moshi.

**WASSIRA AULA**

Katibu huyo alisema NEC imefanya uchaguzi wa wajumbe wa Kamati Kuu ya CCM wawili kwenye nafasi mbili zilizokuwa wazi na amechaguliwa Stephen Wassira na Theresia Mtewele.

**UCHAGUZI CCM**

Kuanzia Julai 2, mwaka huu, fomu za kuwania nafasi ngazi ya Wilaya, Mkoa na Taifa zitatolewa hadi Julai 10, mwaka huu.

## Mbunge aendeleza moto wa kikokotoo aliouwasha Bulaya

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

MBUNGE wa Jimbo la Ngara, Ndaisaba Ruhoro, ameiomba serikali kuachana na mpango wa utekelezaji wa kikokotoo kipya cha asilimia 33 ifikapo mwaka 2023.

Aidha, amesema kasi ya watumishi waliofikisha umri wa kustaafu kuomba kustaafu kwa hiyari ni kubwa kwa sababu wanawahi kabla hakijaanza kikokotoo kipya.

Akichangia mjadala wa makadirio ya bajeti ya serikali kwa mwaka wa fedha 2022/23 jana, alisema ni vizuri kikokotoo kipya kikaacha kutumika na kurudi cha zamani cha asilimia 50.

"Eneo la kikotoo linaleta presha kubwa sana kwa watumishi nchini hasa wanaokaribia kustaafu, watumishi wote Tanzania wana taarifa kwamba 2023 ndiyo mwisho wa kuahirishwa kikokotoo kilichokuwa kimeletwa na kikapandisha joto nchini.

"Sasa hivi kila mtumishi ambaye umri wake umekaribia kustaafu wala hasubiri, ukifika muda wake wa kustaafu kwa hiyari haraka anamtafuta mbunge anawasilisha nyaraka zake anastaafu kukimbia kikokotoo mwaka 2023.

"Naomba hicho kikokotoo ki 'rest in peace' (kipumzike kwa amani) huko huko ambako kilipelekwa kisirudi tena kwa sababu hadi sasa kinaleta joto kubwa na presha kwa Watanzania."

Kwa mujibu wa sheria ya hifadhi ya jamii, muda wa kustaafu kwa hiyari ni miaka 55 na kwa lazima miaka 60, huku maprofesa na madaktari wakiwa ni miaka 60 ya hiyari na 65 ya lazima.

Ushauri wa Mbunge huyo umekuja siku moja baada ya Mbunge wa Viti Maalum, Ester Bulaya, kutaka serikali kuachana na kikokotoo cha asilimia 33 na kuendelea cha 50, kwa kile alichodai kinampunja mtumishi.

Mjadala wa kikokotoo uliibuliwa na gazeti hili mwaka 2017, baada ya kuandika ripoti ikionyesha fomu ya mafao ilivyo kwenye kanuni za sheria ya hifadhi ya jamii za mwaka 2018, iliyotaka kuleta usawa kwa wastaafu wa sekta binafsi na serikali.

Sheria iliyounganisha na kubakiwa na mifuko miwili ukiwamo wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), unaohudumia sekta binafsi, ilikuja na kanuni ambazo zilitaka kuleta usawa wa mafao kwa mifuko yote.

Sheria iliyounganganisha mifuko ya PPF, PSPF, LAPF na GEPF kuwa PSSSF, ilipitishwa na Bunge Oktoba 20, mwaka 2017 kuunganisha mifuko na kufanya marekebisho kwenye Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), kuwa mahususi kwa ajili ya wafanyakazi wa sekta binafsi na sekta isiyo rasmi.

Sheria hiyo ilianza kazi Agosti mosi, 2018 na ndiyo ilikuwa tarehe rasmi ya kuanza kwa mfuko wa PSSSF na kanuni zake zilishatangazwa kwenye gazeti la serikali.

**ALICHOKISEMA NDALICHAKO**

Serikali imewataka Watanzania kuacha kusikiliza maneno ya upotoshaji kuhusu mfumo huo mpya wa kulipa mafao ya wastaafu nchini.

Waziri wa Nchi Ofisi ya waziri mkuu Kazi, Ajira na Watu wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako alibainisha hayo jana jijini Dodoma alipokuwa akifungua mkutano mkuu wa chama cha waajiri nchini (ATE).

Alisema kumekuwapo na maneno ya upotoshaji kuhusu kikokotoo kipya na kuwataka Watanzania kuyapuuza.

**MSTAAFU ATOA YA MOYONI**

Mwalimu Mokima Ng'nondwa wa Tabata Liwiti, jijini Dar es Salaam, aliishukuru Nipashe kwa kazi nzuri ya kutetea maslahi ya wafanyakazi kwa kupitia gazeti lao kutokana na kuchapisha taarifa iliyohusisha kikokotoo fao NSSF.

Alisema kazi hiyo ilitakiwa ifanywe na wawakilishi wao ikiwamo Chama cha Walimu Tanzania (CWT), lakini wamekaa kimya.

HABARI KITAIFA

# Wanne walivyofariki ajali ya treni

**Na Mwandishi Wetu**

WATU wanne wakiwamo watoto wawili wamefariki dunia na wengine 132 kujeruhiwa katika ajali ya treni ya abiria iliyokuwa ikisafiri kutoka Kigoma kwenda Dar es Salaam.

Taarifa ya Shirika la Reli Tanzania (TRC) iliyotolewa jana imeeleza kuwa treni hiyo ya abiria yenye namba Y14 ilitoka Kigoma juzi, saa mbili usiku na kupata ajali eneo la Malolo, mkoani Tabora saa tano asubuhi.

"Treni hiyo iliondoka Stesheni ya Kigoma majira ya saa mbili usiku, siku ya Jumanne Juni 21,2022 kuelekea Dar es Salaam ikiwa na behewa nane zilizobeba abiria 930, ilipofika eneo la Malolo mabehewa matano ya abiria daraja la tatu, behewa moja la vifurushi, la huduma ya chakula na vinywaji na la breki ziliianguka na kusababisha ajali," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Majeruhi 132 wa ajali hiyo wamepelekwa katika Hospitali ya Mkoa ya Kitete mkoani humo na wanaendelea vizuri.

"Ajali imesababisha vifo vinne wakiwamo watoto wawili, wa kike mwenye umri wa miaka mitano na wa kiume miezi minne na watu wazima wawili mwanaume na mwanamke," ilisema taarifa hiyo.

Shirika linaendelea na zoezi la kuwasafirisha manusura wa ajali kutoka Tabora ili kuendelea na safari ya kuelekea Dar es Salaam.

Shirika linaendelea kufuatilia kwa karibu kufahamu chanzo cha ajali ili kuchukua hatua.

**Majeruhi 132 wa ajali hiyo wamepelekwa katika Hospitali ya Mkoa ya Kitete mkoani humo na wanaendelea vizuri.**

# Utata waibuliwa bungeni zabuni ujenzi wa SGR

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

MBUNGE wa Jimbo la Biharamulo (CCM), Ezra Chiwelesa, ameitaka serikali kuangalia zabuni iliyotengwa kwa ajili ya ujenzi wa kipande cha reli ya kisasa (SGR) kutoka Tabora hadi Kigoma, huku akionyesha wasiwasi wa matumizi ya 'single sourcing'.

Akichangia mjadala wa mapato na matumizi ya serikali kwa mwaka 2022/23, mbunge huyo alisema utaratibu wa kupanga bei elekezi kwenye manunuzi ya umma ni kutengeneza wizi mpya kwa kuwa vifaa au mashine zinatofautiana bei kutoka nchi moja hadi nyingine.

"Nina uzoefu kwenye hivi vitu hasa ukifanya manunuzi ya kiufundi, leo unataka kununua excavator kuna ya China, katapila na nyingine, utakapotaka kupanga tuwe na bei elekezi ni kukaribisha wizi, zinatoka nchi mbalimbali na viwango tofauti," alisema.

Alisema mtu akishajua analeta mashine ya Kichina ambayo ni Dola 120,000 na ameshajua bei elekezi ni Dola 180,000 atapandisha bei inafika 165,000.

"Kama wafanyakazi wetu wanashida tutafute mbinu nyingine, sidhani kama sheria ina shida, shida ni hao wanaotuhudumia kesho ukibadilisha sheria watakuja na mambo mengine, ninaomba vitu kama 'restricted tendering' na 'single sourcing' vinasababisha matatizo haya," alisema na kuongeza:

Juni 14, mwaka huu, katika hotuba ya Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alilieleza Bunge kuwa serikali imeanza mchakato wa kutafuta mkandarasi wa kujenga kipande cha reli ya kisasa cha Tabora hadi Kigoma, kilomita 514 kwa Dola bilioni 2.1.

Mbunge Chiwelesa alisema ukibadilisha Dola bilioni 2.1 kwenda kwenye shilingi ni Sh. trilioni 4.851.

"Ukifungua mfumo wa TANeP walifanya 'single sourcing' na inafanyika ukifungua mkandarasi wa China Civil Engineering Construction Corporation (CCECC), ambaye amepitishwa peke yake ana Sh. trilioni 6.698, tofauti ni nini, kati ya anachokisema waziri hapa na waziri amesha 'tender' kwenye mfumo ni Sh. tril. 1.847 huku waziri alisema Sh. trilioni 4.8.

"Hii tofauti ni kuanza na sala na tunasema Mungu atusaidie kwenye maamuzi ya walio wengi, sioni kama kuna maamuzi ya walio wengi, ninachoomba tulichukuwe kwasababu waziri amesema na mchakato unaendelea."

"Tulichukue aliye 'tender' (zabuni) kwa 'single source' ana asilima 38 zaidi ya ambayo waziri aliyosema, hakuna atakayepunguza kwa asilimia hizo, tumekuwa wafanyabiashara na wote tunajua.

"Ninaomba hili jambo kama taifa na kwa maslahi ya wengi tuliangalie lisije likatuangusha kwasababu kinachoonekana hata kama anatengeneza faida, huyu mtu hata kama alikuwa na biashara za mabilioni huwezi kuweka faida ya zaidi ya asilimia 50.

"Serikali iliangalie hili jambo, tukatae hii zabuni hizi 'restricted' na 'single source' ndiyo zinasababisha haya. Hapa hizi fedha unazungumzia bajeti za Wizara ya Miundombinu, Mifugo na bajeti nyingine hata ukiunganisha nyingine tatu," alisisitiza.

Alishauri mchakato kuanza upya ili kupata bei ambayo waziri ameitaja bungeni, na kwamba kufanya kwa kadri mzabuni anavyotaka sio sawa kabisa.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Lawrence Mafuru (kulia) na Balozi wa Umoja wa Falme za Kiarabu nchini Tanzania, Khalifa Abdulrahman Almarzooqi, wakisaini nyaraka za makubaliano ya ushirikiano wa kiuchumi ili kuhamasisha, kulinda uwekezaji na kutotoza kodi mara mbili kwa ajili ya kuzuia ukwepaji wa kodi ya mapato, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Msako mkali wahamiaji haramu Loliondo

**Na Novatus Makunga,** LOLIONDO

KAMISHNA Jenerali wa Uhamiaji nchini (CGI) Dk. Anna Makakala, ametangaza operesheni maalumu ya siku 10 ya kuwasaka wageni wote walioingia nchini na kuishi bila ya kufuata taratibu za uhamiaji katika eneo la Loliondo lililoko wilayani Ngorongoro, Mkoa wa Arusha.

Kamishna Jenerali Dk. Makakala, alitangaza msako huo katika ziara ya kikazi kufuatilia zoezi linaloendelea la uwekaji wa mawe ya mpaka katika pori tengefu la Loliondo eneo la kilometa za mraba 1,500.

Tayari kuna taarifa za wageni wa nchi jirani kuingia na makundi ya mifugo na kuwa moja ya sababu ya taharuki katika eneo la Loliondo hasa katika pori tengefu.

"Tunaanza rasmi operesheni ya kuwasaka wahamiaji haramu ambao wapo nchini hususani eneo la tarafa ya Loliondo kinyume cha sheria kuanzia leo (jana)," alisema.

Akizungumzia changamoto ya Jeshi la Uhamiaji la uwezo wa rasilimali watu, fedha na vifaa, Dk. Makakala alisema wamejiandaa kuendesha operesheni hiyo kwa ufanisi na lengo likiwa ni endelevu baada ya hizo siku 10.

Dk. Makakala alisisitiza kufuatwa kwa sheria za nchi wageni wanapotaka kuingia au kutoka nchini na kwamba Uhamiaji imejipanga vyema kusimamia eneo hilo katika mipaka yote nchini.

"Nchi yetu imebarikiwa kwa kuwa na maeneo mazuri ambayo yanavutia wahamiaji haramu kufika nchini kwa sababu tofauti, hatutakubali hilo litokee wakati wowote ule," alisema Makakala.

Mkuu wa Wilaya ya Ngorongoro, Raymond Mangwala, alibainisha tatizo la wahamiaji haramu katika wilaya hiyo limekuwa kubwa na operesheni hiyo imekuja wakati muafaka.

Mangwala alifafanua kuwa mazoezi mawili tofauti yanayoendelea katika wilaya hiyo ambayo la kwanza ni kuondoka watu kwa hiari katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na la pili la uwekaji wa mpaka katika pori tengefu la Loliondo.

Alisema kuwa hadi kufikia mwishoni mwa wiki iliyopita waliohama kwa hiari kutoka tarafa ya Loliondo kwenda kijiji cha Msomera Wilaya ya Handeni Mkoa wa Tanga walikuwa watu zaidi ya 110 kutoka katika familia 21.

Alisema katika wiki zinatarajiwa kuhama familia 27 kati ya hizo tatu hazitaenda kijiji cha Msomera badala yake zimejitafutia maeneo mengine baada ya kulipwa fidia nzuri na serikali.

Mangwala alisema kwa upande wa tarafa la Loliondo zoezi linaloendelea ni la uwekaji wa mawe ya alama za mpaka katika pori tengefu la Loliondo katika ukubwa wa kilometa za mraba 1,500 kati ya eneo lote la kilometa za mraba 4,000.

"Katika tarafa ya Loliondo hakuna mtu aliyeondolewa wala kuhama kwani zoezi haligusi maeneo ya makazi bali eneo la uhifadhi kwa kuwekwa mpaka huku wananchi wakiachiwa eneo la kilometa za mraba 2,500 kwa ajili ya makazi, ufugaji na kilimo," alisema.

# TEF yalaani mgambo wa Jiji kubugudhi wauzaji magazeti

**Na Mwandishi Wetu**

JUKWAA la Wahariri Tanzania (TEF) limeeleza kusikitishwa na vitendo vilivyofanywa na askari wa Jiji la Dar es Salaam vya kuwanyanyasa na kuchukua meza za wauzaji magazeti wanaofanya shughuli zao maeneo mbalimbali ya jijini.

TEF imesema matukio hayo ya uonevu dhidi ya wauzaji magazeti, yamethibitishwa kufanywa na mgambo wa jiji dhidi ya wauzaji magazeti bila kuwapo sababu zilizoainishwa kufanya hivyo.

Taarifa iliyotolewa na Mwenyekiti wa Jukwaa hilo, Deodatus Balile jana, ilibainisha kuwa, Oktoba mwaka jana serikali ilianza kuwaondoa wafanyabiashara wadogo pembezoni mwa barabara za jiji hilo, lakini wauzaji magazeti hawakuondolewa kutokana na sababu za msingi.

"Siyo kwamba hawakuondolewa kwa bahati mbaya, bali waliachwa kwa mujibu wa Sheria ya Ongezeko la Thamani (VAT) ya Mwaka 2014, nyongeza ya 9(3) inayotambua magazeti kuwa ni nyenzo ya elimu siyo biashara," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema sheria hiyo inafanana na sheria karibu zote za kodi ya mapato na Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) duniani kote, na ndiyo maana katika miji yote kuna meza za magazeti na vitabu katika kona za mitaa kwa ajili ya kuendeleza elimu na maarifa kwa watu wake.

"Tanzania itakuwa nchi pekee duniani kuzuia watu wake wasisome magazeti na vitabu kwa kuingiza uuzaji huu wa nyenzo za elimu katika orodha ya biashara kama kitendo kilichofanywa na mgambo wa Jiji la Dar es Salaam," alisema.

Balile alisema mbali na kueleza masikitiko hayo, TEF linamtaka Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji hilo na wengine wenye nia kama hiyo ya kubughudhi wauza magazeti, kusitisha mara moja mpango wa kuondoa meza za wauza magazeti na kuwarejeshea meza zao walioporwa. Alisema pamoja na kuwarejeshea meza zao pia Jiji linapaswa kuwaomba radhi Watanzania kwa uamuzi huo wa kuwakosesha nyenzo muhimu ya kujielimisha iliyoruhusiwa kwa mujibu wa sheria.

"Kuruhusu uamuzi huu kuendelea ni sawa na kuamua kwa makusudi kujenga taifa lenye kizazi cha watu wajinga, kwani maarifa yanapatikana kwa kusoma magazeti na vitabu, tunamwomba Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, kuchukua hatua za haraka kusitisha kadhia hii inayovunja sheria za nchi," Balile alisema.

Mwenyekiti huyo alisema wahariri wanalaani kitendo hicho na kusisitiza kamwe kisirudiwe tena kwa kuwa kwa mwelekeo huo, mgambo wanataka kulisukuma taifa katika kujaribu ujinga ambao una gharama kubwa kwa sasa na baadaye.




Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA), Hamza Johari, akimkabidhi kwa niaba, kitabu mmoja wa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Minazi Mirefu. TCAA imekabidhi vitabu 467 vya masomo mbalimbali kwa shule hiyo iliyoko Kata ya Kipawa jijini Dar es Salam, ikiwa ni sehemu ya kurudisha huduma kwa jamii (CSR) inayoizunguka. **PICHA: DICKSON MULASHANI**

# Gari la shule lilivyoua mwanafunzi nyumbani

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MWANAFUNZI wa Chekechea mwenye umri wa miaka minne, aliyekuwa akisoma katika Shule Binafsi ya Msingi Samuu iliyoko Manispaa ya Shinyanga, amefariki dunia kwa kugongwa na basi la shule hiyo, mara baada ya kumshusha nyumbani kwao.

Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, George Kyando, alisema jana kuwa tukio hilo limetokea juzi majira ya saa 12 jioni wakati dereva wa basi hilo lenye namba za usajili T 151 DAG, lililokuwa likiendeshwa na Kassim Mahona (40), lilipokuwa linageuzwa.

Alisema dereva huyo wakati akimshusha mwanafunzi huyo nyumbani kwao, Mtaa wa Majengo Mapya, Manispaa ya Shinyanga, alipokuwa akigeuka ndipo alipomgonga mtoto huyo.

"Dereva wa basi hili tunamshikilia kwa ajili ya kujibu mashtaka yanayomkabili ya kumgonga mwanafunzi na kusababisha kifo chake," alisema.

Kamanda Kayando alisema chanzo cha ajali hiyo ni uzembe wa dereva kwa kutochukua tahadhari kwa watumiaji wengine wa barabara.

Alitoa wito kwa madereva wote wa vyombo vya moto mkoani humo, kuzingatia sheria za usalama barabarani ili kutosababisha ajali zisizo za lazima zitokanazo na uzembe.

# Wanawake waongoza matumizi dawa kulevya

**Na Vitus Audax,** MWANZA

JESHI la Polisi mkoani Mwanza limesema idadi ya wanawake wanaotumia dawa za kulevya mkoani humo, imeongezeka maradufu kulinganishwa na wanaume.

Akisoma taarifa ya mwenendo wa vitendo vya matumizi ya dawa za kulevya mkoani Mwanza katika utangulizi wa Siku ya Kupambana na Dawa za Kulevya, Mrakibu wa Jeshi la Polisi, Denis Rwiza kutoka Ofisi ya Ushirikishwaji wa Jamii wa jeshi hilo, alisema kati ya Februari hadi Mei mwaka huu, idadi ya watumiaji wa dawa za kulevya kwa wanaume imepungua kulinganishwa na wanawake inayozidi kupanda.

Mrakibu Denis alisema idadi ya wanaume waliokamatwa kwa matumizi ya dawa za kulevya katika miezi hiyo ni 132 kulinganishwa na mwaka jana walikuwa 174.

Alisema idadi ya wanawake waliokamatwa katika kipindi kama hicho, mwaka huu ni 22 wakati mwaka jana walikuwa 10.

"Kwa hiyo kuna ongezeko la watu 12 huku wanaume idadi ikipungua kwa watumiaji 42," alifafanua.

Alisema kuwa bangi imezidi kuongoza ambapo mwaka huu wamekamata kilogramu 410, ikilinganishwa na kilogramu 207 zilizokamatwa mwaka jana.

"Misokoto ya bangi tumekamata gramu 580 ikilinganishwa na gramu 963.5, sawa na kupungua kwa asilimia 39.9. Miche ya bangi iliyokamatwa ni 1,264 ikilinganishwa na 1,259 iliyokamatwa mwaka jana, sawa na ongezeko la miche mitano ambayo ni asilimia 0.39 iliyokamatwa kwa mwaka 2021," alisema.

Kwa upande wa mirungi, Mrakibu Denis alisema wamekamata kilogramu 442 kutoka kilogramu 993 zilizokamatwa mwaka jana ikiwa ni sawa na kupungua kwa asilimia 10.3, heroine gramu 2.5 ikilinganishwa na gramu 4.5 zilizokamatwa mwaka 2021.

Alisema heroine imepungua zaidi kutokana na udhibiti wa usafirishaji uliofanywa kupitia juhudi za wadau mbalimbali pamoja na Jeshi la Polisi.

Maadhimisho ya Siku ya Kupambana na Dawa za Kulevya yanatarajiwa kufanyika kitaifa Julai 2 mwaka huu mkoani Dar es Salaam, yakiwa na kauli mbiu 'Tukabiliane na dawa za Kulevya kwa Ustawi wa Jamii'.

# Mufti Mkuu ahimiza chanjo UVIKO-19

**Na Beatrice Shayo**

SHEIKH Mkuu wa Tanzania, Mufti Abubakar Zubeir, amewaagiza masheikh wote kuanzia ngazi za kata kuwaelimisha waumini umuhimu wa kuchanja ili kujikinga na ugonjwa wa UVIKO-19 na kwamba huduma hiyo itaanza kupatikana baada ya sala ya Ijumaa katika misikiti yote.

Mufti Zubeir aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa mafunzo kwa viongozi wa dini ya Kiislamu kuhusu ugonjwa huo, ili nao wakawaelimishe waumini wao umuhimu wa kuchanja.

Alisema mafunzo hayo yanalenga kuwajengea uwezo viongozi wa dini ili wakawahimize waumini wao kuchanja ili wajikinge na hatari ya kupata maambukizi ya ugonjwa huo. "Chanjo ni jambo la muhimu ninawahimiza watu wote wajitokeze kuchanja kwa sababu ni jambo ambalo halina tatizo kwenye dini yetu. Tumewahimiza masheikh wawahamasishe na kuwapa maelekezo waumini wachanje," alisema.

Mufti alisema awali kulikuwa na upotoshaji kwa watu kuchanja chanjo hiyo, lakini wahusika waliokuwa wakipotosha nao wamejitokeza kuchanja baada ya kupata uelewa.

Alisema chanjo hiyo haina madhara yoyote na imethibitishwa na wataalamu, hivyo mtu anapopatiwa chanjo hiyo ni rahisi kujikinga na kuzuia maambukizi kwenda kwa mwingine.

Mtendaji Mkuu wa Shirika la Management and Development For Health (MDH), Dk. David Sando, alisema wamekutana na viongozi wa juu wa dini ya Kiislamu, masheikh wa mikoa, wilaya na kata kwa ajili ya kuangalia juhudi za kutekeleza mpango wa Wizara ya Afya wa kuongeza idadi ya watu waliopata chanjo ya UVIKO-19.

"Tumeona ni namna gani tunaweza kushirikiana na dini hii ya Kiislamu kuwafikia kwenye jamii ili kufikisha elimu kuhusu hii chanjo na kuongeza kasi ya kuchanja, hivyo tunaamini kabisa kwa taarifa iliyotolewa na Mufti na mwongozo wa vipindi vinavyofuata kwa sasa kwenye semina, vitajenga uwezo wa masheikh na viongozi wa dini ya Kiislamu kwa Mkoa wa Dar es Salaam," alisema.

Alisema MDH imejipanga kuhakikisha timu za wachanjaji zinakuwapo hadi ngazi ya jamii na tayari wana timu ya watu zaidi ya 300 ambao wametapakaa katika mkoa mzima kuhakikisha kila anayehitaji kuchanja, anapatiwa katika eneo lake la makazi.

Dk. Sando alisema wataanza kuziweka huduma hizo katika nyumba za ibada na tayari viongozi wengine wa dini wameshawajulisha ili kuongeza uhamasishaji kwa wananchi. "Lengo kubwa la leo ni kuhakikisha kwamba kuanzia wiki hii na kuendelea baada ya ibada ya Ijumaa kunakuwa na vikundi vya uchanjaji kwenye misikiti ili kutoa huduma kwa waumini," alisema.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Rashid Mfaume, alisema kwa mkoa huo lengo lao ni kuchanja watu milioni 3.8 na hadi jana, tayari wamechanja zaidi ya watu milioni 1.4.

Alisema mkakati ulioko ni kuongeza kasi ya uchanjaji kwa ajili ya kujikinga na aina nyingine ya kirusi ambacho hawajui kitakuja lini, hivyo kama watu wakichanja hata kikija kirusi kipya, madhara ya ugonjwa hayatakuwa makubwa.

# RC apokea taarifa mzee aliyetoweka miaka 10

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MFANYABIASHARA maarufu wa mjini Singida anadaiwa kumteka na kumficha kusikojulikana kwa zaidi ya miaka 10 sasa, mtu aliyekuwa mfanyakazi wake, ambaye haijulikani kama yupo hai au amefariki dunia.

Madai hayo yalitolewa jana na mkazi wa mkoani hapo, Omari Rashid mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Bilinith Mahenge, kwenye mkutano wa kusikiliza kero za wananchi uliofanyika katika viwanja vya stendi ya zamani Manispaa ya Singida.

Rashid ambaye alidai ni mtoto wa mtu huyo aliyetekwa, alidai kuwa baba yao hajaonekana tangu mwaka 2010 baada ya mfanyabiashara huyo kumlaghai na kuchukua hati ya nyumba yao na kisha kuwafukuza katika nyumba hiyo na sasa wanaishi kwa kutangatanga.

Aliongeza kuwa mfanyabiashara huyo aliyemtaja kwa jina, alimrubuni baba yao kwamba atamlea na familia yake kwa kipindi chote cha maisha yao, lakini katika hali ya kushangaza, wamejikuta wakitimuliwa na mfanyabiashara huyo ambaye amejimilikisha nyumba yao iliyoko eneo la Majengo, Manispaa ya Singida.

Rashid alisema kinachowashanga na kujiuliza maswali yasiyo na majibu ni kwamba baba yao hajaonekana tangu mwaka huo hali inayowafanya waingiwe na hofu kama yupo hai au ameshafariki dunia.

"Mheshimiwa RC (Mkuu wa Mkoa), utatusaidiaje jambo hili ili tupate nyumba yetu na tujue hatima ya baba yetu alipo?" Alihoji.

Kufuatia ombi hilo, Mkuu wa Mkoa Singida, Dk. Mahenge alimwagiza Katibu Tawala wa Wilaya ya Singida na Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Lucas Mwakatundu, wachukue maelezo ya kina ya mlalamikaji huyo ili serikali iyafanyie kazi.

Dk. Mahenge aliwaagiza viongozi kuanzia ngazi za wilaya hadi chini kujenga tabia ya kuitisha mikutano ya wananchi na kusikiliza kero zao.

Alitumia nafasi hiyo kuwaeleza wananchi mafanikio mbalimbali yaliyofanywa na serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Alisema katika kipindi cha mwaka mmoja wa uongozi wa Rais Samia, Mkoa wa Singida umepatiwa Sh. bilioni 230 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji, barabara, elimu na umeme.


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**MAOMBI YA TAARIFA YA KUONESHA NIA KWA AJILI YA USAMBAZAJI WA MAGARI YA KUJIPAKIA SARUJI NA KUCHANGANYA ZEGE KWA AJILI YA MRADI WA EACOP KUMBUKUMBU NA: 0010007759**

EACOP Limited (Kampuni) Tanzania, kampuni ya Mafuta , inakaribisha na inaalika taasisi/kampuni zenye weledi na uzoefu kuonesha nia ya kutoa huduma ya kusambaza Magari ya kujipakia saruji na kuchanganya zege kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba lililofukiwa chini la kusafirisha Mafuta linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalo safirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Mkoa wa Tanga, Tanzania kwa ajili ya kusafirisha Mafuta katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:**

- EACOP inahitaji huduma za taasisi/kampuni zenye weledi na uzoefu kuonesha nia ya kutoa huduma ya kusambaza Magari ya kujipakia saruji na kuchanganya zege
- Aina ya magari yatakayopendekezwa yanatarajiwa kuwa na uwazo wa kupakia jumla ya saruji, mchanga, kupima kundi, kuchanganya saruji, usafirishaji, na kuiweka popote inapohitajika. Kwa hivyo ni mashine ya kusimama pekee ambayo inaweza kukamilisha kazi ya kuchanganya saruji kwa kutumia mwendeshaji mmoja mwenye uzoefu kwa mashine na kusafiri chini ya nguvu zake.
- Takriban magari tisa (9) ya kujipakia yenyewe ya kujipakia yatahitajika; hasa ya ukubwa wa aina mbili tofauti mbili yaani mita za ujazo 3.0 na uwezo wa mita za ujazo 4.5.
- Msambazaji/ wasambazaji watatakiwa kuwa na uwezo wa kutoa magari yote tisa (9) ya kujipakia ndani ya kipindi cha juu cha siku 100 za kupokea agizo
- Magari ya saruji ya kujipakia yatakodishwa na kupelekwa katika Mikoa inaypoitiwa na Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) katika mikoa nane (8) tofauti; Kagera, Tabora, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Manyara na Dodoma

**VIGEZO MUHIMU:**

Kwa sababu ya ukubwa wa upeo na kusaidia kampuni zinazoonyesha nia, Mradi unahifadhi haki ya kutoa vifurushi vya kazi ya mtu binafsi na/au vifurushi vingi vya kazi kwa msambazaji anayestahiki.

Makampuni yanayovutiwa yanaweza kuingia katika makubaliano na makampuni mengine ili kuboresha uagizaji wa huduma zao hata hivyo, wote na kila mshirika katika makubaliano LAZIMA atimize mahitaji yaliyoainishwa hapa chini.

Makampuni/Mashirika yanayoonyesha nia yanaalikwa kutuma maombi pamoja na nyaraka zifuatazo:

- Uzoefu, utendaji na uwezo katika kutekeleza majukumu yaliyoainishwa chini ya maelezo ya huduma, kwa kiwango kikubwa nchini Tanzania, kwa kuzingatia viwango vya kitaifa na kimataifa (pamoja na Viwango vya Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC), wenye uzoefu wa angalau miaka 10 ya utendaji wa huduma sawa na iliyoainishwa katika upeo wa kazi.
- Uwezo wa kuzalisha mita za ujazo 3.0 kwa saa pamoja na miundo mingine yenye ujazo wa mita za ujazo 4.5 kwa saa
- Uwezo wa kupewa leseni ya kusafiri barabarani nchini Tanzania
- Mfumo wa taa za barabarani
- 4x4 - Uendeshaji wa magurudumu manne, na usukani wa kaa
- Kwenye mfumo wa maji bodi ndani ya gurudumu yenye uwezo wa kuchanganya zege, pampu ya maji moja kwa ajili ya gurudumu la zege
- Gurudumu la zege yenye skrubu za kuchanganya na lenye uwezo wa kupima uzito
- Kupakua vipakuzi kwa kutumia viendelezi na uwezo wa kupima uzito
- Gurudumu la kuchanganya zege iliyofungwa yenye viwango vya ROPS na FOPS kiwango cha kwanza · Udhamini na waranti unaojumuisha masaa 2000 za kazi/ mwaka 1
- Mafunzo ya Opereta
- Seti ya huduma kwa mwaka 1 ikijumuisha matairi ya ziada
- Uwezo wa kuhudumia na kudumisha upakiaji wa magari ya saruji yanayojifunga yenyewe yenye vipuri na lori linalotembea la huduma/karakana uliomo ndani ya nchi (Tanzania.
- Mafundi waliohitimu na wenye uzoefu wa kukarabati na kutunza magari inapohitajika
- Kazi muhimu za wafanyikazi waliohitimu na uzoefu zilizoainishwa chini ya wigo wa kazi kwa miradi ya mafuta na gesi ambayo inatii mahitaji ya IFC.
- Wasilisha/Thibitisha uzoefu wa kusimamia miradi, utaratibu wa ugavi na usafirishaji vitu pamoja na manunuzi · Uwezo wa kifedha wa kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha hesabu za fedha kwa mwaka wa fedha uliopita.
- Inashauriwa, mwonyesha nia atume maombi ya kusajiliwa katika kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia.
- Utoaji wa leseni ufaao kutoka kwa mamlaka husika ndani ya nchi kwa ajili ya utoaji wa huduma.
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya Ndani za mwaka 2017 pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Ndani na sheria za Kitaifa na Kimataifa pamoja na viwango vya Kimataifa vya mafuta na gesi.
- Thibitisha na wasilisha será za Afya, Usalama na Mazingira (HSE/OSHA) na usimamizi wa viwango vya ubora na maswala ya jamii
- Uthibitisho wa usajili katika Mamlaka ya Mapato ya Tanzania (TRA) na Cheti cha Ithibati ya Malipo ya Kodi cha mwaka wa hivi karibuni

Makampuni yenye nia, ambayo yana uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu yanatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia iliyoandaliwa kwa lugha ya kiingereza pamoja na nyaraka tajwa kupitia barua pepe: **procurement.tz@eacop.com** (ukubwa usiozidi **MB20**) hadi kufikia saa **9:00** mchana Majira ya Afrika Mashariki, tarehe **7 Julai 2022** Kichwa cha Barua Pepe ni **0010007759.**

**Muhimu:** Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya makampuni ya Awali yenye vigezo, Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA).

Taarifa ya kuonesha nia iwe kwa lugha ya kiingereza.

216916101

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Dosari hii irekebishwe masoko yawe na faida

**KARIBU** kila mkoa Tanzania Bara sasa kunashuhudiwa kumejengwa au kunajengwa masoko na vituo vya kisasa vya mabasi, ujenzi huo ukigharimu mabilioni ya shilingi.

Hata hivyo, kinyume cha matarajio ya wengi kwamba masoko na vituo hivyo vingelikuwa na manufaa kwa Taifa kiuchumi, imebainika kwa sasa kwenye baadhi ya mikoa, hakuna faida inayopatikana kutokana na uwekezaji huo.

Mathalani, katika ukaguzi wa kitaalamu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ambao ripoti yake inafanyiwa kazi na Bunge kwa sasa, imebainika masoko na vituo vya mabasi havijawa na matokeo chanya kimapato.

CAG katika ukaguzi wa ufanisi kwenye usimamizi wa masoko na vituo vya mabasi nchini, ameweka bayana kwamba ameshindwa kuiona faida ya uwekezaji huo wa zaidi ya Sh. bilioni 530 kwenye miradi hiyo.

Kimsingi, kanuni za uanzishaji wa serikali za mitaa zinatamka bayana kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa zina jukumu la kudhibiti na kusimamia masoko na vituo vyote vya mabasi.

Hata hivyo, kilichobainika kuwa nyuma ya kutoonekana faida kwenye uwekezaji huo, ni usimamizi mbovu wa masoko na vituo vya mabasi unaochagizwa na: Kukosekana kwa umakini wakati wa kufanya upembuzi yakinifu; mazingira yasiyoridhisha ya utendaji kazi; ukosefu wa ofisi za wasimamizi wa masoko na kutokuwapo kwa mikataba ya upangaji.

Vilevile, zipo dosari zingine zinazojumuisha migogoro ya ardhi iliyochangiwa na ukosefu wa hatimiliki na kuwapo kwa viongozi wa umma ambao hawafanyi kazi kwa manufaa ya umma, hivyo kuchangia usimamizi hafifu katika uendeshaji wa masoko na vituo vya mabasi.

Nipashe tunaona kuna haja kumulika vikwazo tajwa ili masoko na vituo vya mabasi viwe na tija ikizingatiwa kwamba uwekezaji katika miradi hiyo umegharimu zaidi Sh. bilioni 530, ambazo ni mali ya umma, huku baadhi ya miradi ikibainika haitumiki kikamilifu.

Ripoti ya CAG inabainisha masoko na vituo vya mabasi vyenye dosari hizo, likiwamo Soko la Chuno katika Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani lililojengwa chini ya mradi wa Miji ya Kimkakati Tanzania kwa gharama ya Sh. bilioni 5.54 huku makadirio ya makusanyo yake kwa mwaka yakiwa Sh. milioni 138.1.

Inashtusha pale inapobainika soko hilo lina vibanda 237 vilivyo wazi kwa zaidi ya miezi minne na kusababisha hasara ya mapato ya Sh. milioni 32 huku masoko ya Skoya na Chiyangu pamoja na Kituo cha Mabasi cha Chipuputa katika Manispaa hiyohiyo ya Mtwara-Mikindani yakiwa wazi kwa kipindi cha mwaka mzima na kusababisha hasara ya jumla Sh. milioni 131.


Kwa kuzingatia uzito wa suala hili, Nipashe tunaona kwamba suala la kutotumika kwa masoko na vituo vya mabasi vilivyojengwa lisiposhughulikiwa ipasavyo na kwa wakati, linaweza kuchelewesha kupatikana kwa faida itokanayo na uwekezaji mkubwa uliofanywa.

Ni rai yetu kwa mamlaka husika kuchukua hatua kwa kuwa kutotumika kwa miundombinu hii kutasababisha uchakavu na hivyo kushusha thamani yake.

Hivyo, tunaishauri serikali kupitia menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa, kuimarisha usimamizi wa mfumo wa masoko na vituo vya mabasi kwa kuhakikisha wafanyabiashara wote wanatumia masoko na vituo vya mabasi vilivyojengwa badala ya kutumia maeneo yasiyo rasmi ili kupata thamani ya fedha za miundombinu iliyojengwa.

Kuepuka hasara tajwa, Nipashe pia tunaona kuna haja serikali ihakikishe upatikanaji wa huduma za kijamii na kiuchumi kama vile umeme, maji, idadi ya watu, makazi na mengine yanayofanana na hayo, uzingatiwe wakati wa upembuzi yakinifu kwa kuwa kuwapo kwake kunatengeneza mazingira mazuri ya kuvutia biashara.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Kichwa kikubwa na mgongo wazi visiwe vikwazo vya kupata elimu



Na Sabato Kasika

**BAADHI** ya wanafunzi wenye ulemavu kila mara hukumbana na vikwazo kadhaa katika kufikia malengo yao waliyojiwekea kupitia elimu, hali ambayo wakati mwingine inaweza kuwakatisha tamaa.

Miongoni mwa hao wenye ulemavu wanaokumbana na hayo ni wenye shida ya kuwa na kichwa kikubwa au mgongo wazi, ambao inaelezwa wanakataliwa usajili katika baadhi ya shule za serikali.

Watoto hao hupata shida hizo, hasa baada ya serikali kuanzisha utaratibu wa elimu jumuishi, inayolenga kuwafanya wanafunzi wenye ulemavu na wale wazima kusoma pamoja.

Hata hivyo, kumekuwapo madai kwamba, watoto wenye ulamevu wa kichwa kikubwa na mgongo wazi, wanakataliwa kuandikishwa kuchangamana na wenzao wenye viungo kamili.

Madai hayo yanatolewa na Mwenyekiti wa Chama cha Wazazi wa Watoto Wenye Kichwa Kikubwa na Mgongo Wazi Tanzania (ASBAHAT), Abdul-hakim Bayakub na anaiomba serikali iwasaidie kumaliza tatizo hilo.

Ni katika mkutano wa chama hicho na wadau wengine wa elimu, anatoa malalamiko hayo na kufafanua kuwa elimu jumuishi ilianzishwa, ili wanafunzi wote wakiwamo wenye ulemavu na wasio na ulemavu, wasome pamoja darasa moja.

Ni vyema basi wanaowanyima fursa watoto hao wahitaji wakatafari kwa umakini, hata kuchukua hatua sahihi za kutowatenga watoto wenye ulemavu, kwani hawakuomba wazaliwe hivyo.

Pia bado inabaki kuwa busara kukumbuka msemo wa Kiswahili kwamba 'hujafa hujaumbika.' Hivyo, kila mmoja kati yetu ni mlemavu mtarajiwa, kwani anaweza kukumbwa na madhila au ugonjwa unaompa hali ya ulemavu.

Inawezekana mazingira kama hayo ya kuzuia yakawafanya baadhi ya wazazi kuacha kuwapeleka watoto wenye ulemavu shuleni, kwa kuhofia kuchekwa, kudharaulika, au kushushiwa heshima.

Vilevile, mazingira hayo ya mizengwe kwa namna moja au nyingine, yanaweza kukwamisha lengo la kuwapo elimu jumuishi, ambalo ni kuwafanya wanafunzi wote bila kujali ulemavu, kusoma pamoja.

Nadhani walimu kama walezi, wangesaidia au kuwa chachu kuondoa vikwazo hivyo, ili kuhakikisha wanafunzi wenye ulemavu wanapata elimu na wenzao wenye viungo kamili, ili iwasaidie katika maisha yao ya baadaye.

Kuwajumuisha wanafunzi katika elimu, kunahitaji ushirikiano na taasisi mbalimbali kama za kiafya, kijamii, ustawi wa jamii, maji na usafi wa mazingira, usafiri wa umma na sekta zinazohusiana na haki.

Ninaamini kwamba, wadau hao wote wakishiriki kwenye jambo hili, inaweza kusaidia kumaliza vikwazo wanavyokumbana navyo watoto wenye ulemavu hasa wa kichwa kikubwa na mgongo wazi vya kukataliwa kuandikisha shule.

Pamoja na hayo, ninaamini pia kuna haja ya kuwekeza katika kuongeza ubora wa majengo, vifaa vya kujifunza na kufundishia katika shule zetu, ili kuwasaidia wanafunzi wenye ulemavu, ambao serikali imeamua kuwajumuisha na wenzao kupata mafunzo kwa pamoja.

Ulemavu huo wa kuwa na kichwa kikubwa na mgongo wazi, kuna wakati Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, ameshawahi kutolea ufafanuzi, kwamba watoto wenye hali hiyo wanaendelea kupokelewa shuleni, pia serikali inajitahidi kuboresha miundombinu ya shule zote zinazojumuisha watoto wenye ulemavu.

Wakati fulani ameshawahi kutoa mfano, kwamba Shule ya Sekondari Patandi, iliyoko Arusha ni ya mfano, kwa vile inachukua wanafunzi wote wakiwamo wenye ulemavu, huku ikiwa na walimu wenye utaalamu wa kuwafundisha wanafunzi wenye hali hiyo ya dosari kiafya. Ingekuwa vyema, kama shule zinazodaiwa kuwakataa watoto wenye ulemavu huo kuzingatia kile ambacho waziri, ameshawahi kukieleza kuhusu ujumuishaji wa watoto hao, ili kuondoa mkanganyiko uliopo.

Ikumbukwe kwamba, viongozi wa ASBAHAT wanabainisha kuwapo wenye ulemavu huo, ambao wamesoma na kuhitimu masomo yao vizuri na sasa wanategemewa katika taasisi mbalimbali za umma na binafsi katika utaalamu tofauti, ukiwamo wa TEHAMA.

Mafanikio hayo yangewafanya walimu wanaowakataa walemavu wa kichwa kikubwa na mgongo wazi wabadili mtazamo na kutambua kuwa wana uwezo mzuri shuleni kama walivyo wengine wenye viungo kamili.

## Mbunge: Ni sahihi mikopo halmashauri kupunguzwa

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

MBUNGE wa Nyasa, Stela Manyanya, ameunga mkono kupunguzwa kwa mikopo itakanayo na mapato ya ndani ya halmashauri kwenda kwa makundi maalum kutoka asilimia 10 hadi tano.

Akichangia mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya serikali kwa mwaka 2022/23 jana, tofauti na wabunge wengine walichangia mjadala huo tangu Juni 16, mwaka huu, waliotaka serikali kutogusa asilimia 10 na badala yake waiongeze, alisema:

"Kwa bahati nzuri eneo hili nimelifanyia kazi kwa kipindi kirefu, kundi la machinga siyo wale wanaotembea tu, wametoa jina hilo kutokana na ubunifu wao wa kufanya biashara kiasi kwamba hata wajasiriamali wadogo wenye mtaji kuanzia Sh. 1,000 hadi milioni 50 wanaangukia kundi hilo.

"Niliwahi kusema iko haja ya kuiga mtindo tunaowafanyia nyuki, tunawatengenezea mzinga wanakupa asali, na hawa machinga wanafanya kazi ambazo ukijumlisha katika thamani ya kazi wanayofanya ni fedha nyingi na wanatengeneza ajira nyingi sana.

"Lakini kwa sababu kundi hili hatujalitambua kamili na kulipa haki kamili ya maeneo ya kufanyia kazi, ndiyo maana wakati mwingine tunampa presha Rais kwamba wamachinga wapate maeneo ya kufanyiakazi, wote (wabunge) tunachangia humu.

"Leo linapokuja suala la sasa tuanze kutengeneza mazingira bora ya hawa watu kufanyia kazi, wote (wabunge) tunaruka, tunasema bora wakakopeshwa.

"Lakini mimi niwaambie ukweli hata katika baadhi ya maeneo ufuatiliaji wa waliokopeswa, ni mgumu kwa sababu hawajulikani waliko, watu wanapewa fedha kwenye kikundi wanagawanagawana, mambo yameisha zinakuwa kama fedha za msaada badala ya kuwa fedha za kuwawezesha katika masuala ya kibiashara.

"Haya nasemea mimi kama mimi, nasimama mimi kama mimi, najua wabunge wengi wamekuwa upande tofauti lakini kazi ya mbunge ni kila mtu anashauri anavyoona."

Mbunge huyo alisema wazo la kupunguza asilimia tano kwenda kwenye miundombinu ni zuri na linatakiwa kuanza kwa baadhi ya maeneo.

"Mimi ningetamani jimbo langu la Nyasa liwe mfano, na mimi naunga mkono asilimia tano ikatengeneze miundombinu na asilimia tano wakopeshwe na watakaokosa waende benki kwa sababu zipo," alisisitiza.

Katika mchango wake, Mbunge wa Ngara, Ndaisaba Ruhoro, alisema wameshaonja bei ya Sh. 3,740 kwa kilo na kama haitashuka kwenye soko la dunia, hawatauza kahawa kwa bei ya chini kwa kuwa zao hilo siyo nyanya wala biringanya kwamba litaoza, bali wahifadhi ndani hadi bei nzuri itakapopatikana.

# Auawa kwa mapanga nyumbani kwa hawara

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

MKAZI wa Kijiji cha Kiziwa, Kata ya Kiroka wilayani Morogoro, Kibwana Mussa, amekutwa ameuawa kwa kukatwa kwa mapanga nyumbani kwa mwanamke anayedaiwa kuwa na uhusiano naye kimapenzi.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kiziwa, Mbena Loki, alisema jana kuwa mkazi huyo aliuawa na mtu aliyedaiwa alikuwa mume wa mwanamke huyo aliyemtaja kwa jina la Farida Ally.

Alibainisha kuwa walipata taarifa za kuuawa kwa mwanaume huyo Juni 22, mwaka huu.

Mwenyekiti huyo alisema viongozi mbalimbali wa kijiji walikuwa eneo la tukio na kumchukua mwanamke huyo na kumpeleka kituo kidogo cha Polisi Mkuyuni kwa ajili ya usalama wake.

Kiongozi huyo wa kijiji alisema anachofahamu mwanamke huyo alikwishaachana na mume wake muda mrefu na alikuwa kwenye uhusiano na mwanamume aliyeuawa.

"Mtuhumiwa alikuwa bado akimfuatilia mwanamke na leo akamvizia na kumkuta ndani na kuamua kumuua mwanamume aliyemkuta ndani kwa kumkata kwa mapanga," alidai mwenyekiti huyo.

Inadaiwa kuwa baada ya kufanya mauaji hayo, mtuhumiwa huyo alikimbia kusikojulikana na jitihada zaidi za kumtafuta bado zinaendelea.

Mwili wa marehemu tayari umeshaondolewa kijijini huko na kupelekwa hifadhi maiti ya Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro ili kusubiri taratibu zaidi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Fortunatus Musilimu, alikiriri kutokea kwa mauaji hayo Juni 22 majira ya saa 11 alfajiri katika Kitongoji cha Kiziwa na kwamba chanzo cha mauaji hayo ni wivu wa kimapenzi.

Alisema Jeshi la Polisi linamtafuta mtuhumiwa wa mauaji hayo aliyefahamika kwa jina la Ally Ally, mkazi wa Kibwala, Kiziwa wilayani Morogoro kutokana na kudaiwa kuhusika na mauaji hayo.



Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Hashimu Mgandilwa (kushoto), akipokea zawadi ya diary yenye kalenda na ratiba ya masomo na matukio mbalimbali ya mwaka mzima ya Chuo cha Tumaini, Dar es Salaam kutoka kwa Waziri wa Utawala Bora serikali ya wanafunzi TUSODARCO, Isaya Daniel. Wanafunzi hao walikuwa kwenye utalii wa ndani katika mapango ya Amboni yenye lengo la kuunga mkono jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan kuboresha sekta ya utalii nchini. **PICHA: MARIA RAYMOND TUDARCO**

## Serikali yasisitiza kuheshimu taratibu, sheria za wakimbizi

**Na Faustine Feliciane**

WIZARA ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imesema itaendelea kuheshimu makubaliano ya kimataifa kuhusu wakimbizi na haitotoa shinikizo kwa wakimbizi kuondoka nchini bila hiari yao.

Wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Wakimbizi Duniani, jijini Dar es Salaam jana, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, alisema Tanzania itaendelea 'kufungua milango' yake kwa watu wanaokimbia nchi zao na kutafuta usalama nchini.

"Kama taifa milango ipo wazi raia wa kigeni wanaokimbia vurugu nchini mwao, Tanzania tutaendelea kufuata makubaliano ya kimataifa juu ya wakimbizi, lakini tutaendelea kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia wakimbizi (UNHCR)," alisema Mulamula.

Alisema mpaka kufikia Mei mwaka huu, Tanzania ina wakimbizi 243,077 kutoka Burundi wanaoishi kwenye makambi mbalimbali.

Mwakilishi wa UNHCR nchini, Mahoua Parums, alisema wanaishukuru Tanzania kwa kuwa sehemu salama kwa wakimbizi wanaokambilia nchini.

"Tanzania ina historia ndefu na wakimbizi, UNHCR tunaishukuru Tanzania kwa ushirikiano na ukalimu unaotoa kwa wakimbizi, na kama alivyosema Waziri Mulamula, hakuna mkimbizi atakayelazimishwa kurudi nchini kwake kama hakuna uhakika wa usalama," alisema Mahoua.

Mwakilishi Mkazi wa Umoja wa Mataifa (UN), Zlatan Milisic, alisema wanatekeleza mradi wa pamoja wa Kigoma ambao unawanufaisha wananchi wa mkoa huo na wakimbizi walioko kwenye makambi yaliyoko Kigoma.

Balozi wa Comoro nchini, DK. Ahamada El Badaoui Mohamed, alizitaka nchi za Afrika kuimarisha amani ili kupunguza na kuondoa wakimbizi Afrika.

Hafla hiyo ya maadhimisho ya Siku ya Wakimbizi Dunia iliandaliwa na UNHCR kuhudhuriwa pia na wakuu wa mikoa ya Kigoma, Tabora na Rukwa.

# Tembo waua mzee akiokoa mbaazi zake

**Na Stevie Chindiye,**
TUNDURU

MKAZI ya Kijiji cha Kajima, Kata ya Kajima wilayani Tunduru mkoani Ruvuma, Mohammed Jusso (65), amefariki dunia baada ya kushambuliwa na tembo.

Taarifa za tukio hilo zinaeleza kuwa mzee huyo alipatwa na mkasa huo wakati akiwafukuza tembo hao ili waondoke katika shamba lake la mbaazi.

Shuhuda wa tukio, Sadala Mapunda, alisema lilitokea juzi majira ya saa mbili usiku, akisimulia kuwa baada ya tukio hilo, wananchi waliojitokeza na kwenda kuokoa mwili wa marehemu usiendee kushambuliwa na tembo hao na baadaye kutoa taarifa kwa viongozi wa serikali kwa ajili ya taratibu za kisheria.

Diwani wa Kajima, Ausi Maulid, alisema tayari amekwishatoa taarifa kwa maofisa wanaohusika na uhifadhi wa wanyamapori.

Diwani wa Viti Maalum Tarafa ya Matemanga, Stawa Timamu, alitumia fursa hiyo kuiomba serikali kuwasaidia kuwahamisha wafugaji wanaokaa kwenye maeneo ya misitu ya hifadhi ili pindi wanyama hao waharibifu wanapofukuzwa, waende kukaa huko tofauti na sasa ambapo kila tembo wanapofukuzwa kwenda huko hurudi tena kwenye makazi ya wananchi kwa kuyakimbia makundi ya ng'ombe hao.

Ofisa Tarafa ya Matemanga, Emiliani Njogopa, alisema kuwa baada ya tukio hilo, aliwasiliana na askari wa hifadhi za jamii ambao walikwenda kutoa msaada wa awali kwa kuwafukuza tembo na kutoa nafasi kwa wananchi kuchukua mwili wa ndugu yao na kuupeleka nyumbani.

Ofisa Wanyamapori Wilaya ya Tunduru, Limbega Alii, alithibitisha kuwapo kwa tukio hilo na tayari amekwishapeleka askari wa kikosi cha idara hiyo kwa ajili ya kuwafukuza tembo hao katika maeneo ya makazi ya wananchi. Limbega aliwataka wananchi wa maeneo hayo kufanyia kazi maelekezo yanayotolewa na wataalamu, ikiwamo kutembea zaidi ya mtu mmoja pamoja na kuacha tabia za kuwafukuza tembo hao huku wakiwa wamewasha tochi, hali ambayo huonyesha huwa wanajimulikia.

Alisema hili ni tukio la tatu kwa tembo hao kuua watu mwaka huu, hali ambayo inatishia maisha ya wananchi wengi endapo jamii haitabadilisha tabia.




Mwakilishi wa Barron Group of Companies, Jacqueline Kawishe (nguo ya njano), akimkabidhi Mwenyekiti na Mwanzilishi wa Taasisi ya Mwanamke Initiatives Foundation (MIF), Wanu Hafidh, viatu vya shule vya Barron vilivyotolewa na Shule ya Feza, jijini Zanzibar juzi, kama mchango wao katika mfuko wa MIF. Wengine ni wajumbe wa Bodi ya MIF. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbunge aona mbinu kuinua uchumi nchini

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

MBUNGE wa Vwawa, Japhet Hasunga, amesema sekta ya kilimo imebeba uhai wa taifa na ndiyo njia sahihi ya kuwekeza kwa sasa ili nchi ipate mapato makubwa na kuondokana na umaskini.

Hasunga alibainisha hayo bungeni juzi alipochangia hoja ya mapendekezo ya bajeti ya serikali kwa mwaka 2022/23, akisema:

"Kwenye kilimo ndipo panapatikana chakula chote, bila chakula hakuna kazi inayoweza kufanyika. Sote tunategemea chakula lakini ndipo tunapata malighafi zote za viwanda na ndipo penye ajira nyingi."

Mbunge huyo alisema uwekezaji kwenye sekta ya kilimo utaipatia nchi fedha nyingi za kigeni na kuiwezesha kulipa madeni mengi ya nje, hivyo kuna haja kuweka mkazo kwenye sekta hiyo.

Vilevile, alisema uwekezaji wa taifa lazima utegemee kwenye kilimo, uvuvi, ufugaji na misitu kwa kuwa ndiko kwenye fursa za biashara kwani Watanzania wengi wanaishi kijijini na wanategemea biashara hiyo.

Akizungumzia sekta ya utalii, Hasunga alisema inaweza kuleta mchango mkubwa katika nchi kama ikishirikiana vizuri na sekta zingine za uzalishaji.

"Utalii kwa mwaka uliopita 2021 duniani pamoja na kuwapo kwa ugonjwa wa UVIKO-19, zipo nchi zimefanya vizuri sana. Lakini ukichukua takwimu za namna ya vivutio vya utalii vizuri, Tanzania tulikuwa tunashika nafasi ya pili duniani, sasa hivi tumeshuka hadi nafasi ya nane," alisema.

Hasunga alisema licha ya nchi kufanya vizuri, uwekezaji wake hautoshi kwa kuwa bado haijapata watalii wa kutosha, hali inayosababisha kutopata mapato mengi.

Aliirejelea Ufaransa kuwa kwa mwaka 2021, ilipata watalii milioni 89.4 ikifuatwa na Hispania iliyopata watalii milioni 83.7 huku Marekani ikipata milioni 79.5 wakati Tanzania bado haijafikia idadi ya watalii milioni moja.

"Lazima tuwekeze vya kutosha, ndiyo maana Rais wetu ameamua kuja kuhakikisha anaisimamia hii sekta vizuri, akaja na huu utaratibu wa filamu ya Tanzania The Royal Tour. Kwa kweli hii filamu inatutangaza sana kama nchi, na mimi ninafikiri tujipange kuhakikisha utalii unaleta mchango mkubwa," alisema.

Hasunga alisema kuna haja nchi iwekeze zaidi kwenye hoteli ili watalii wengi wanaokuja kwenye shughuli mbalimbali, wafikie kwenye hoteli hizo ili wailetee nchi fedha nyingi za kigeni pamoja na kuhamasisha utalii wa ndani. "Ndio maana mwaka 2018 nilisema kwa mara ya kwanza kuwa Watanzania tujifunze kula maisha, twende tukale maisha kwenye mbuga zetu.

"Watanzania wengi hawakunielewa wakadhani ni utani, hiyo ni theory (nadharia) ya kiuchumi. Ili uchumi wetu uchangamke, Watanzania tukale maisha," alisema Hasunga ambaye mwaka 2018 alikuwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii.

## Wananchi kunufaika na miradi ya maji

**Na Frank Monyo**

WATANZANIA zaidi ya milioni mbili wanaoishi katika sehemu zenye shida katika upatikanaji wa maji, wamenufaika na miradi ya maji inayofadhiliwa na Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL).

Msaada huo unakuja wakati takwimu zinaonyesha zaidi ya watu billioni mbili duniani hawapati huduma ya majisafi na salama huku nchi zinazoendelea zikiathirika zaidi.

Wakati wa kukabidhi mradi wa maji katika Kata ya Basutu wilayani Hanang' juzi, Mkurugenzi wa Uhusiano kwa Umma wa SBL, John Wanyancha, alisema kusaidia upatikanaji wa majisafi na salama umekuwa ni moja ya vipaumbele vya kampuni hiyo, akibainisha kuwa imechimba visima 20 kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Alisema kampuni hiyo inachukulia maji kama moja ya mahitaji muhimu kwa maendeleo ya watu na ndiyo sababu imekuwa mstari wa mbele kushirikiana na serikali na wadau wengine kusaidia upatikanaji wa majisafi na salama kwa Watanzania.

Mkurugenzi huyo alisema miradi ya maji ya SBL imesaidia upatikanaji wa maji na salama kwa takriban watu milioni mbili na kuongeza kuwa miradi hiyo imelenga zaidi jamii ambazo zina uhitaji mkubwa wa huduma hiyo muhimu na ambazo zinaishi jirani na viwanda vyao au sehemu ambayo SBL inapata malighafi kwa ajili ya uzalishaji wa bia.

Alisema kuwa mbali na miradi ya maji, kampuni hiyo pia imesaidia kuboresha afya za wakazi wa maeneo husika.

"Pamoja na kusaidia jamii zenye shida ya maji moja kwa moja, miradi yetu pia imekuwa ikizisaidia taasisi mbalimbali za kijamii na mfano mzuri ni mradi wa Karatu ambao umepanuliwa na kutoa huduma kwa shule nne na kituo cha afya wakati mradi wa Pasua Moshi, umesaidia upatikanaji wa maji kwa shule tatu na soko lililoko jirani," alisema Wanyancha.

Alisema: "Miradi yetu huwa jirani na maeneo ambayo SBL hununua nafaka kwa ajili ya utengenezaji wa bia, husaidia kuwapatia wakulima zaidi ya 400 maji kwa ajili ya umwagiliaji.

"Wakulima hawa pia wapo katika mpango unaojulikana kama 'Kilimo Biashara na SBL', huwasaidia kuongeza uzalishaji kwa kuwapatia mbegu bora, ushauri wa kitaalamu na kuwaunganisha na taasisi za kifedha kwa ajili ya kupata mitaji ya kupanua uzalishaji wao."

Kwa mujibu wa Taasisi ya Water Org inayofanya kazi ya kusaidia upatikanaji wa maji na usafi wa vyoo, zaidi ya asilimia 57 ya Watanzania, sawa na watu milioni 25 kati ya watu milioni 57 wanaokadiriwa kuwapo nchini, wanaweza kupata maji kupitia vyanzo vilivyoboreshwa huku asilimia 30 wakipata huduma ya vyoo safi.



Mbunge wa Jimbo la Morogoro Mjini, AbdulAziz Abood (watatu kushoto), akimwonyesha Mhandisi wa Ujenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, Juma Wizo, eneo la stendi ya Bajaji nje ya soko kuu la Kingalu ili lijengwe vyoo, mbunge huyo amejitolea kujenga vyoo na kuweka taa katika eneo hilo. **PICHA: ASHTON BALAIGWA**

# Profesa UDSM ahimiza utafiti kusaidia jamii

**Na Gwamaka Alipipi**

MKURUGENZI wa Shahada za Awali katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) ameitaka Ndaki ya Sayansi Asili na Sayansi Tumizi ya chuo hicho (CoNAS) kufanya utafiti wenye kuleta maendeleo ili kusaidia jamii.

Profesa Nelson Boniface alitoa ushauri huo jana jijini Dar es Salaam wakati wa mwendelezo wa sherehe za miaka 60 tangu kuanzishwa kwa UDSM zinazotarajiwa kufikia kilele Oktoba mwaka huu, akimwakilisha Makamu Mkuu wa chuo kikuu hicho, Prof. Willium Anangisye.

Prof. Boniface alisema: "Mnapofanya utafiti, hakikisheni unaleta manufaa katika uchumi wa nchi sambamba na kusaidia jamii. Kama utafiti wetu mnaofanya hauegemei katika mambo hayo mawili, basi utakuwa hauna maana. Mnatakiwa kufanya utafiti utakaowakwamua wananchi, mkishafanya msizifungie kabatini."

Alisema CoNAS ilianzishwa mwaka 1965, yaani miaka minne baada ya kuanzishwa kwa UDSM, ikiwafundisha walimu wa masomo ya sayansi na tangu kipindi hicho, imekuwa ikifanya utafiti mbalimbali wenye manufaa ikiwamo utafiti wa mafuta katika mimea na kuvuna uyoga.

Prof. Boniface aliutaka uongozi wa CoNAS kujikita zaidi katika kufanya utafiti wenye ubunifu na sayansi za maendeleo, akisisitiza dunia inakwenda kwenye teknolojia ya sayansi na ubunifu.

Mkuu wa Ndaki ya CoNAS, Prof. Flora Magige, alisema tangu kuanzishwa kwa ndaki hiyo, wanajivunia mafanikio lukuki katika nyanja ya utafiti wa kisayansi.

Alisema mojawapo ya mafanikio makubwa wanayojivunia ni kugundua dawa ya kutibu ugonjwa wa virusi vya corona iitwayo UDANO ambayo iliwatibu wagonjwa wengi wakati wa mlipuko wa ugonjwa huo.

Prof. Magige alisema: "Tangu mwaka 1965 hadi sasa, tunajivunia kuongezeka kwa usahili wa wanafunzi wanaojiunga katika ndaki yetu. Hata idadi ya wafanyakazi imeongezeka, tulivyoanza sivyo tulivyo sasa, hata utafiti nao umeongezeka, tumefanya mengi yenye manufaa kwa jamii na taifa."

Alisema CoNAS bado inaendelea katika kufanya utafiti na ubunifu wenye matokeo chanya kwa taifa na jamii, kwamba kwa miaka ijayo Watanzania watarajie mambo mazuri zaidi.

# Teknolojia ya kuua mbu wa malaria, dengue yaja

**Na Romana Mallya**

TEKNOLOJIA ya kupambana na mbu waenezao ugonjwa wa malaria na homa ya dengue, ikiwaua ikitumika ndani na kuwafukiza inapopulizwa nje ya nyumba.

Mkuu wa Ujumbe wa Kampuni ya Fumakilla Limited, Toshiaki Muramoto, alibainisha hayo juzi baada ya kutembelea Tanzania kwa ajili ya tathmini ya mahitaji inayoungwa mkono na Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan (JICA).

Katika ziara hiyo, wajumbe hao walitembelea maeneo ambayo yameathirika zaidi na malaria na dengue na ilikuwa ya kwanza tangu kuidhinishwa kwa mradi wa Fumakilla kama Mpango wa Ushirikiano wa JICA wa mwaka 2019.

Muramoto alisema Fumakilla imekuwa ikitengeneza viuadudu vya nyumbani kwa zaidi ya miaka 100 na wamepanga kuanzisha teknolojia ya hali ya juu ya kupambana na mbu.

"Teknolojia hii ni kwa ajili ya kupambana na malaria, homa ya dengue na magonjwa mengine ya kuambukiza yanayohusiana na mbu nchini, tutafanya hivyo kwa kushirikiana na JICA," alisema.

Muramoto alisema bidhaa hiyo mpya hutoa moshi kidogo wa kuua mbu inapotumika ndani ya nyumba na inafukuza mbu inapotumiwa nje.

"Koili mpya ya mbu ni bidhaa yenye ufanisi dhidi ya mbu wa kienyeji, imepata kiwango cha juu cha usalama ambacho kimeainishwa kama Daraja la U (haiwezi kuleta madhara makubwa) na Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO). Ni uainishaji wenye moshi kidogo, zaidi ya hayo, bei yake itakuwa nafuu kwa watu wengi," alisema.

Muramoto ni Mjapan aliyefanya utafiti wa mfumo wa kilimo katika Mkoa wa Morogoro kwa takriban mwaka mmoja, miaka 27 iliyopita kwa msaada wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA).

"Nilipokuwa kijijini, nilitembelea mashamba kila siku kuwahoji wakulima na kukusanya udongo kwa ajili ya majaribio ya kimaabara.

"Nikiwa nafanya kazi shambani niliumwa na mbu na nikaugua malaria mara tatu ndani ya mwaka mmoja na kulazwa hospitalini mara mbili," alibainisha.

Alisema baada ya kumaliza masomo yake, alirudi Japan na kuamua kufanya kazi katika kampuni ya Fumakilla na kuona ipo haja ya kuitambulisha koili iliyotengenezwa kwa teknolojia ya hali ya juu inayoua mbu kama bidhaa muhimu ya kudhibiti mbu.

Alisema bidhaa hiyo tayari imefanyiwa majaribio na kuidhinishwa na Taasisi ya Utafiti wa Viuatilifu vya Kitropiki (TPRI), wakala wa serikali ambao wanadhibiti matumizi ya viua wadudu Tanzania.

Alisema utafiti wa tathmini ya mahitaji ya Fumakilla, ukiungwa mkono na JICA, ulianza Oktoba 2020 na utakamilika mwaka 2023, kwa ziara tatu zaidi zilizopangwa nchini Tanzania.

Alisema wakati wa ziara yao, ujumbe ulifanya mijadala ya vikundi na jumuiya za wenyeji ili kuangalia utangamano wa ndani wa bidhaa hizo na ilizitoa kwa wakazi kwa ajili ya majaribio ya matumizi ya nyumbani.

"Maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya utafiti huo ni mikoa ya Dar es Salaam, Kilimanjaro, Arusha, Dodoma, Pwani, Mwanza na Mtwara," alisema.

Aliongeza kuwa timu yao ilifanya vikao vya kushauriana na maofisa wa serikali wanaosimamia udhibiti wa vijidudu vya magonjwa katika Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kuhusu uwezekano wa kutumia bidhaa hiyo kama njia ya kudhibiti.

# Mbunge atoa mamilioni kukarabati kituo cha Bajaj

**Na Christina Haule,** MOROGORO

MBUNGE wa Morogoro Mjini, Abdulaziz Abood, ametoa zaidi ya Sh. milioni 10 kwa ajili ya kukarabati Kituo cha Bajaj cha Soko Kuu la Chifu Kingalu ambacho kwa sasa hakina huduma ya choo.

Akizungumza kituoni hapo jana baada ya kujionea hali halisi, Abood alisema ameamua kutoa kiasi hicho cha fedha ambacho kitasaidia maboresho ya stendi hiyo ikiwamo ujenzi wa choo, ujenzi wa daraja na ufungaji wa taa kwa ajili ya usalama nyakati za usiku.

Mhandisi wa Manispaa ya Morogoro, Juma Wizo, alisema ujenzi huo utaanza muda si mrefu baada ya michoro kwenye eneo hilo kukamilika.

Awali madereva wa bajaj wanaofanya safari kwenye maeneo ya Chamwino, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Kasanga na Mzumbe, akiwamo Abdallah Malilo, walimshukuru mbunge huyo kwa kuona umuhimu wa kuwatatulia baadhi ya kero wanazokumbana nazo kwenye stendi hiyo.

Alisema uwekaji wa taa kwenye eneo hilo utawasaidia hasa wanapofanya shughuli zao nyakati za usiku kwenye kupakia na kushusha abiria sambamba na kuimarisha usalama kwao na abiria na mali zao.

Dereva huyo alisema kuna kero nyingine ya ufinyu wa eneo hilo unaoleta shida kutokana na wingi wa bajaj kwenye eneo hilo, akiomba Manispaa kuangalia uwezekano wa kuwatanulia eneo hilo ili liwe kubwa zaidi kukidhi mahitaji yao.

Malilo alisema eneo hilo linapakana na Soko la Mitumba Kikundi ambalo lina eneo kubwa na kwamba ikiwa wataongezwa eneo, watakuwa salama bila kuhofu kuingia Mto Kikundi ambalo upo jirani.

Alisema kwa sasa wengine wanapaki pembezoni mwa mto, jambo ambalo ni hatari, akirejea siku ambayo mmoja wao alinusurika kutumbukia mtoni, akiokolewa na wenzake waliomvuta baada ya bajaj kuingia mtoni.

# Madini Nickel kuichangia Ngara bil. 151/-

BUNGE limeelezwa uchimbaji wa madini ya Nickel utachangia ushuru wa huduma kwa Halmashauri ya Wilaya ya Ngara mkoani Kagera takribani Sh. bilioni 151 kwa kipindi cha uhai wa mgodi.

Naibu Waziri wa Madini, Dk. Steven Kiruswa, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Ngara (CCM), Ndaisaba Ruhoro.

Mbunge huyo alisema, mpango wa serikali kuhakikisha wananchi wa Jimbo la Ngara wananufaika na uchimbaji wa madini ya Nickel unaotarajia kuanza eneo la Kabanga.

Akijibu, Dk. Kiruswa alisema uchimbaji wa madini ya Nickel katika eneo la Kabanga unafanywa na Kampuni ya Tembo Nickel Corporation Limited iliyopewa leseni Oktoba 25, 2021.

"Mradi huo unatarajia kuchangia ushuru wa huduma kwa Halmashauri ya Wilaya ya Ngara, kiasi cha Dola za Marekani milioni 65, sawa na takribani Sh. bilioni 151 kwa kipindi cha uhai wa mgodi," alisema.

Alisema mradi huo unatarajia kutoa ajira za moja kwa moja 978.

"Hadi kufikia Aprili, 2022 mradi ulikuwa umetumia jumla ya Dola za Marekani milioni 1.5 katika ununuzi wa bidhaa na huduma ndani ya nchi. Kati ya hizo, Dola za Marekani 125,673 zilitumika kufanya ununuzi katika Wilaya ya Ngara," alisema.

Alitoa rai kwa wananchi wa Wilaya ya Ngara na taifa kwa ujumla kuchangamkia fursa zilizoko katika mradi huo.

"Kupitia Sheria ya Wajibu wa Makampuni kwa Jamii (CSR), mradi huo ulichangia takribani Sh. milioni 39 kwa mwaka 2021 na unatarajia kuchangia Sh. milioni 207.8," alisema.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo alihoji kama Wizara ya Madini ina tafiti zilizofanywa na wakoloni za madini ili kuwekwa wazi kwa Watanzania wawekeze.

Dk. Kiruswa alijibu kuwa Wajerumani walipofanya utafiti wa madini nchini waliacha takwimu za kutosha na zipo kwenye wizara hiyo.

Alitoa rai kwa Watanzania wenye nia ya kuwekeza kwenye madini taarifa zipo za tangu mwaka 1925 wazifuatilie ili kuwaongoza kwenye uchimbaji wa madini husika kwenye maeneo yaliyofanyiwa utafiti.



Spika mstaafu wa Bunge ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Kongwa, Job Ndugai (kushoto), akijadiliana jambo na Mbunge wa Jimbo la Mpwapwa, George Malima, walipokutana ndani ya ukumbi wa Bunge kwenye mkutano wa saba kikao cha 48 bungeni jijini Dodoma jana.
**PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mbunge aomba serikali kujenga bwawa la Yongoma

MBUNGE wa Viti Maalum, Naghenjwa Kaboyoka, ameitaka serikali kujenga bwawa la Yongoma wilayani Same ambalo lilifanyiwa michoro ya awali mwaka 1984 ili kuongeza kilimo cha umwagiliaji kwenye eneo hilo.

Akiuliza swali bungeni jana, mbunge huyo alihoji lini serikali itakuwa tayari kujenga bwawa hilo.

"Kwa kuwa bwawa la Karemae lililoko Same Mashariki lilijengwa na wakoloni 1956 na limejaa tope na limesababisha wakulima wa kata ya Kalemawe, Kihulio na Bendera kushindwa kufanya kilimo, je, serikali ina mpango gani wa kutoa tope hilo ili likusanye maji kusaidia kilimo cha umwagiliaji?" Alihoji.

Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, alikiri kuwa sanifu na uandaaji wa michoro ya awali ya Bwawa la Yongoma ulifanyika mwaka 1984 na serikali kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japan (JICA).

Alisema bwawa hilo litakapokamilika litahudumia vijiji vya Misufini, Ndungu, Makokane na Mpirani.

"Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Same ipo katika hatua ya awali ya kufanya mapitio ya upembuzi yanikifu na usanifu wa bwawa la Yongoma," alisema.

Alisema baada ya kukamilika kwa mapitio hayo, ujenzi wa bwawa hilo utawekwa katika mpango wa ujenzi kwa mwaka wa fedha 2023/24.

Aidha, alisema serikali inaendelea kuimarisha skimu za umwagiliaji za Same na kwasasa imepeleka mitambo katika skimu ya Ndungu kwa ajili ya kufanya ukarabati wa dharura.

Kadhalika, Mavunde alisema ataelekeza timu ya wataalamu ili kufanya tathmini katika bwawa la Karemae.

# Kiwango ukuaji mikopo sekta binafsi chapaa

WIZARA ya Fedha na Mipango imesema kiwango cha ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi kimeongezeka kufikia wastani wa asilimia 8.4 katika kipindi cha Julai 2021 hadi Aprili 2022.

Naibu Waziri Hamad Hassan Chande, alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Tumbatu (CCM), Juma Othman Hija.

Mbunge huyo alihoji kwa kiasi gani lengo la Benki Kuu la kutoa mikopo kwa sekta binafsi ili kutoa fursa za ajira hususan kwa wafanyabiashara wadogo na wa kati limefikiwa.

Chande alijibu, kiwango hicho kimeongezeka ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.3 katika kipindi cha Julai 2020 hadi Aprili 2021.

Aidha, alisema kuanzia Desemba 2021, ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi ulikuwa zaidi ya asilimia 10 na Aprili 2022, ukuaji huo ulifikia asilimia 13.4.

Awali, alifafanua kuwa Sera ya Fedha ya Mwaka 2021/22 imeainisha shabaha ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi wa asilimia 10.6 ili kuwezesha upatikanaji wa mikopo kwa gharama nafuu na kuongeza ukwasi katika uchumi.

Pia alisema kutokana na utekelezaji wa sera hiyo, kiwango cha ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi kimeendelea kuongezeka.

Hata hivyo, alisema kutokana na mwenendo huo, matarajio ni kwamba lengo la ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi la asilimia 10.6 kwa mwaka 2021/22 litafikiwa na hivyo kuchangia uwekezaji, uzalishaji na kuongeza ajira nchini.




**Habari zote na Augusta Njoji, DODOMA**

ama
ALHAMISI JUNI 23, 2022
AFYA NA MAZINGIRA




Ukurasa 13




Ukurasa 14

# Namna safari ya saikolojia na falsafa inavyoangukia kwenye afya binafsi

**Na Ummy Matinde, SJMC**

KITAALAMU, ikiwamo kutoka maandiko rasmi ya kitaaluma, msamiati 'maadili' una mzozo mkuu wa mafundisho yanayotolewa katika nafasi mbalimbali, hasa katika malezi, kumuelekeza binadamu atende namna inayomjenga kimazingira na kiafya, yeye na jamii nzima.

Maadili yanayohitajiwa na watu wote, kimsingi yanafanana, lakini saikolojia na mazingira yake yanaweza kuwa tofauti kiasi. Ila huwa saikolojia yake inayowakana katika tabia na ufuasi, hubaki kuwa zao chanya na kubwa linalomfaa mtu kwa mengi, iwe kiafya mazingira na hata kiuchumi.

Watu tangu zamani wamekuwa na maadili kwa namna maalum, kulingana na imani kama za dini, utamaduni na falsafa za vikundi vya binafsi.

Kumekuwepo aina nyingi za maadili katika jamii na kwa ujumla inakubaliwa na wanadamu wengi, mtu binafsi na mazingira ya karibu zaidi, hata kiasili.

Aina zote za maadili zinaelezwa huwa zinasaidia kuwapo ushirikiano kati ya watu, kuwezesha maisha katika jamii na kuongoza maisha yao. Mfano hai wa maadili hayo ni katika ngazi za kiakili, kitaaluma na kifamilia.

Kabla ya ujio wa wakoloni wa Kizungu barani Afrika, historia inaonyesha amani ilitawala na maadili ya Afrika yakafuatwa na Waafrika wenyewe.



Ndivyo ilivyo saikolojia na falsafa ya maisha ya kikoloni, ilivyoangukia hatima ya afya. **PICHA: MTANDAO.**

Lakini, saikolojia hiyo ilichukua sura tofauti zaidi panapo ujio wa wageni, kwa sura za wafanyabiashara, wamisionari na wapelelezi kuchukua nafasi.

Walio katika biashara walitambulisha bidhaa zao, pia dini pamoja na lugha kwa jamii za Kiafrika na kwa sababu pesa hazikuwepo wakati huo, walibadilishana bidhaa na wenyeji, kama vile miwani kwa shaba au almasi kwa kioo, mavazi kwa dhahabu.

Ni mpaka sasa, saikolojia hiyo inashuhudiwa katika jamii ikiwamo ya jamii za Kiafrika, kuenda kuvaa mavazi yenye utamaduni wa ugaibuni na hasa nchi za Magharibi, kama vile Bara Ulaya na Marekani.

Falsafa na saikoliojia hiyo ndio ikashika kasi hata katika imani za kidini, kinachoabudiwa na wageni kikachukua nafasi kuengua maadili na imani walozizikuta.

Hivyo basi, wamisionari walihakikisha wanapandikiza imani zao kwa Waafrika ili kulainisha mioyo yao kiimani na kuingiza maadili yao, jambo ambalo matokeo yake yakaingia kwa ndani katika maisha ya Mwafrika.

Ni aina ya mabadikliko yaliyomletea hata mageuzi ya kiafya muumini, kwa namna moja au nyingine, kutokana na mabadiliko ya matendo na nyendo zake. Mathalan, ama mtu kuanza kutumia au kuacha sigara na pombe, daima inagusa hadi mwelekeo wa afya yake kwa namna nyingi.

Wageni hao katika ujio wao walipeleleza mifumo yote ya uongozi wa Afrika kuunda mazingira ya mataifa yao, wakaingiza tawala zao na kuangusha tawala za Afrika.

Kurejea historia, hadi kufika karne ya 15, wapelelezi wa kigeni walifanikiwa kusaidia mataifa yao walikotoka, wakaingiza maadili ya uongozi wao kwa kusainisha mikataba tofauti, ikiwamo ya ulaghai kwa viongozi wa Afrika wasiojua kusoma na kuandika.

Ikisimama tafsiri hata katika hatua, hiyo kunazalisha sura ya imani, saikolojia na afya mpya ya mwenyeji anayebadilika.

Hapo ndio zama kunasikika majina kama ya Mjerumani Karl Peters aliyeingia mkataba dhidi ya mzawa Sultan Magungo wa Msovero, Tanganyika hata akawekwa chini ya utawala wa Mjerumani.

Baada ya kufanyika mkutano wa Berlin, Ujerumani uliofanyika kati ya mwaka 1884 na 1885, Afrika ikagawanywa kwa mataifa ya kizungu, kila dola mtawala mmoja ikawa na himaya yake, ikiwamo Tanganyika chini ya Mjerumani.

Hivyo ndivyo mila na desturi za Afrika zilibadilishwa kwa mara moja na watawala wa Kizungu, wakitaka wenyeji kufuata kile ambacho watawala wao walitaka kitekelezwe.

Waswahili husema 'mazoea yajenga tabia' na ndivyo ilivyokuwa, tabia mpya ikajengwa ndani ya nafsi za Waafrika wengi waliotawaliwa na Wazungu.

Hapo ikaenda mbali kukishuhudiwa maadili mapya yakizaliwa kuanzia mavazi, elimu, mlo, usimamizi wa mwili na nyanja nyenginezo kwa kasi ya teknolojia vinaendelezwa na kuzika maadili na matendo ya asili ya Bara Afrika.

Zao kuu linaloangukia hapo mbali na hali ya kiuchumi ni saikolojia, falsafa na sura kuu ya mwisho afya ya umma inayozaliwa upya

***Makala hii inaegemea tathmini ya kitaaluma ya mwandishi ambaye ni mwanafunzi katika Shule ya Uandishi wa Habari (SJMC) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.***

AFYA

ANENAVYO DK. BARAKA NZOBO:

# Ilivyo afya kinywa na upeo mdogo jamii kuelewa mahali penye shida

**Na Mary Geofrey**

KIMAUMBILE, kinywa cha mwanadamu ni sehemu ya kichwa kikijumuisha taya la juu na chini, ulimi, meno, misuli ya mdomo, matezi ya mate, mlango wa koo, matundu katikati ya pua na taya ya juu, mishipa yote ya fahamu na damu iliyopo maeneo hayo.

Kazi ya meno ndiyo inayomuwezesha kusaidia kupitisha na kuchakata chakula kitakachoenda tumboni, kukamilisha uyeyushaji wake na kufyonzwa kwenye damu, hata kurutubisha mwili.

Anafafanua mate yameundwa kuwa na vimeng'enya vinavyosaidia kulainisha na kuyeyusha chakula. Meno kazi yake ni kutafuna, kusaga na kukata chakula cha kila aina, kiingiacho mdomoni.

Mtaalamu wa Ufuatiliaji na Udhibiti wa Magonjwa kutoka Wizara ya Afya, Dk. Baraka Nzobo, katika mazungumzo na Nipashe, anasema kinywa na meno yake vinamsaidia mwanadamu kuchakata chakula kwenda tumboni, kukamilisha uyeyushaji wake na kufyonzwa kuingia kwenye damu, kisha inaurutubisha mwili.

Anasema mate yana vilainishi vinavyosaidia kumeng'enya chakula na kazi ya meno ni kutafuna, kusaga na kukata chakula kiingiacho mdomoni.

Dk. Nzobo anasema, watu wengi wamepungukiwa uwezo wa kutafuna vyakula, kutokana na kupoteza meno, hali inayochangiwa na sababu kama vile kung'oa meno yaliyotoboka na yanayouma.

Pia, anataja kuwapo ugonjwa wa fizi unaoshambulia mfupa unaoshikilia jino na kulifanya kulegea, hatimaye kung'oka lenyewe au kwenda kung'olewa hospitali.

Daktari huyo anasema, ugonjwa wa kutoboka (kuoza) na magonjwa ya fizi, yanachangia kuwadhuru Watanzania wengi. Anaendelea: "Hapa nchini, watu wengi wenye umri wa miaka 55 na kuendelea.

"Wamepungukiwa uwezo wakutafuna vyakula mbalimbali kutokana na kupoteza meno mdomoni, kutokana na sababu mbalimbali."

Dk. Nzobo anasema ugonjwa wa kutoboka au kuoza meno na yanayohusu fizi, ni baadhi yanayoongoza kuwashambulia Watanzania, akitoa takwimu; kati ya watoto 100 wenye umri hadi kufika miaka mitano, kati ya 40 hadi 60 wameathirika na ugonjwa huo wa kuoza meno.

Hali kadhalika, anatoa wastani kati ya watu wazima 10 wenye umri miaka 55 au zaidi, kuna wanane wana magonjwa ya fizi.



Uhalisia wa meno ya binadamu yenye kasoro katika sura tofauti. **PICHA ZOTE: MAKTABA.**

**WATOTO KUOZA MENO**

Mtaalamu huyo anataja sababu za watu kuoza meno, ni kutokufanya usafi wa kinywa vizuri hasa katika upigaji mswaki, walau mara mbili kwa siku, asubuhi baada ya kunywa chai na usiku kabla ya kulala.

Anataja sababu nyinginezo zinajumuisha ulaji vyakula vyenye sukari nyingi na kunywa vitu vyenye tindikali kila mara.

Pia, anataja visababishi vinginevyo kuwa ni hali ya kusaga meno, pia anachokiita 'mdomo mkavu' na ugonjwa wa fizi unaosababishwa na bakteria waliojificha kwenye utando wa uchafu kati ya jino na fizi.

**VICHOCHEO VINGINE**

Dk. Nzobo anasema, mabadiliko ya kihomoni wakati wa umri wa balehe na wakati wa ujauzito na baadhi ya dawa za kutibu sonona (depression) ya mawazo na shinikizo la damu, zina mchango mkubwa.

Vingine ni sababu za msongo wa mawazo, uvutaji aina zote za tumbaku, magonjwa kama kisukari, Ukimwi na meno yaliyoota vibaya kama vile kubebana au kujipanga vibaya.

"Ukipoteza meno yote mdomoni, utakuwa kibogoyo. Hali hii unakutana nayo kwa watu wazima wenye umri mkubwa kuanzia miaka 55 na kuendelea, wengi wao wamepoteza meno yao kwa sababu ya kuoza kwa meno na magonjwa ya fizi," anasisitiza.

Mtaalamu huyo wa afya Dk. Nzobo, anasema kuna kundi kubwa la wenye mapengo mdomoni, kuanzia wastani wa kukosa meno matano hadi 20, akiwafafanua wenye mapengo makubwa na vibogoyo, wanapata shida ya kutafuna vyakula.

"Kibogoyo ataishia kumung'unya vyakula vile vinavyoweza kumung'unyika," anafafanua Dk. Nzobo, akiwa na maelezo kwamba mwenye mapengo makubwa anakosa uwezo wa kutafuna vyakula vigumu.

Hapo anatoa mfano wa milo yenye shida inajumuisha nyama zenye mifupa, nyama ngumu, mahindi ya kuchoma, miwa na karanga za kukaangwa na miwa.

Dk. Nzobo anaeleza kwamba kutoboka jino ni hali inayoendana na kuwapo maumivu makali wakati wa kunywa vinywaji vya moto au baridi, mfano wa vya moto unywaji chai na uji, pia juisi au soda za baridi, hata raha kugeuka kuwa karaha kwa mnywaji vimiminika hivyo.

**MDOMO USIOFUNGUKA**

Tabibu huyo anasema, baadhi ya magonjwa ya kinywa na meno husababisha mdomo kushindwa kufunguka vizuri, kiasi cha hata mtu hawezi kupitisha kidole chake kuingia mdomoni.

"Hali hii husababisha mtu kushindwa kuingiza chakula mdomoni na kupelekea kutumia uji tu mpaka pale atakapofanyiwa matibabu ya kuufungua huo mdomo," anasema daktari huyo.

Anafafanua kwamba, kuna magonjwa yanayomsababisha mwanadamu ashindwe kabisa kufungua mdomo kupitisha chakula, hata mtu huyo atawekewa mpira puani ili alishwe chakula kwa njia ya mpira.

Baadhi ya magonjwa anayataja ni kama vile; jipu la jino lililokaba njia ya chakula, mvunjiko mbaya wa mfupa wa taya la chini na baadhi ya saratani za kinywa na meno zilizochelewa kutibiwa.



**TIBA SAHIHI ILIVYO**

Dk. Nzobo anasema, huduma ya afya ya kinywa na meno, imo katika huduma za afya zinazotolewa kuanzia ngazi ya msingi hadi kitaifa na kwa sehemu kubwa, ngazi hii ya msingi ya watoa huduma ni matabibu wa meno na madaktari wasaidizi meno, wakati madaktari wa meno wakiwa wachache.

Anasema madaktari wa kinywa na meno (DDS) wanapatikana kwa wingi kwenye Hospitali za Rufani za Mikoa, Kanda na Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Pia, anasema huduma zinazotolewa na madaktari bingwa, zinajumuisha upasuaji mdogo, mkubwa na wa ubingwa wa juu, kuziba jino na matibabu ya mzizi wa jino, tiba ya magonjwa ya fizi, matibabu ya kinywa na meno kwa watoto, kurekebisha mpangilio mbaya wa meno mdomoni na viungo bandia vya kinywa na meno.

Anasema ili kudhibiti uharibifu wa meno, wataalamu hao wanatoa elimu namna ya kuyakinga kwa wananchi wanaotembelea kitengo cha kinywa na meno katika hospitali nchini.

**WAGONJWA WA MENO**

Dementria Lyimo, ni mwaathirika wa tatizo la maambukizi kwenye fizi, anayesema alianza kutoa usaha kwenye fizi na kila alipoenda hospitali, akawa anapewa dawa za kukausha na anaendelea na shughuli zake.

Anaeleza tatizo hilo liliendelea hadi alipoanza kuvimba tezi juu ya kinywa, akawa anaendelea na matibabu ya kawaida kukausha uvimbe, lakini baadaye akagundua tatizo ni kubwa, hata akaenda kumuona daktari bingwa wa meno.

"Nilifika akaanza kuyafanyia usafi, akaniambia nina tatizo la fizi kuoza. Akaning'oa na jino lingine la mbele ambalo nalo lilianza kulegea. Kwa sasa nina mapengo mawili ya meno ya juu ya mbele," anasema, akiwa na mbadala wa meno bandia, akiendelea kufuata ushauri wa daktari kuhusu utunzaji wa kinywa chake, tatizo lisiendelee.

MAZINGIRA

# RC Songwe acharuka uzembe wa maliasili kuharibiwa na wazawa

- Awasimamisha kazi watendaji wa serikali
- Viongozi wa jadi na waomba kuingilia kati



Hali halisi ya maliasili zinazochomwa mkoani Songwe. **PICHA ZOTE: IBRAHIM YASSIN.**

**Na Ibrahim Yassin,Songwe**

SUALA la umuhimu wa utunzaji mazingira katika vijiji mkoani Songwe, limeendeleza sintofahamu, kisa kikuu ni wakazi kutojua umuhimu wake, licha ya elimu kutolewa na viongozi husika, kukishuhudiwa uvamizi na ukataji miti, pia kuharibu rasilimali hizo.

Hapo athari inajitokeza katika uharibifu na kuzorotesha mazingira kwa njia ya kupunguza rasilimali kama vile hewa, maji na udongo na kupotea wanyamapori, uharibifu wa mazingira kwa hasa makazi ya asili na maliasili yanatumiwa vibaya.

Uharibifu wa mazingira uko katika orodha ya vitisho 10 vinavyotajwa na Benki ya Dunia, pia Umoja wa Mataifa na mashirika yake ya Rasilimali Duniani, Mpango wa Mazingira na Mpango wa Maendeleo, zote zikitoa ripoti kwa umma kuhusu afya na mazingira duniani, mnamo Mei Mosi, mwaka 1998.

Kuhusu mazingira na afya ya binadamu, sehemu maalum katika ripoti hiyo inaeleza jinsi magonjwa yalivyo na mtazamo uliopo, ni iwapo kuna marekebisho makubwa katika afya ya binadamu, maana yake mamilioni ya watu wataishi muda mrefu na wenye afya bora.

Katika Ziwa Rukwa, tarafa ya Kwimba, wavuvi wanalia kukosa kitoweo, huku halmashauri yao kupitia kata ya Udinde, ikikosa mapato kutokana na samaki kutoweka, vijana wengi wanakimbilia kwenda kuvua Sumbawanga.

Wilayani Mbozi, kijijini Nyamwaga penye msitu wa asili, nako imekatwa na kutumika kuchoma mkaa.

Msitu wa Longort, wenye miti mingi ya aina tofauti na ya asili, nao umeharibiwa na miti yake kuchomwa mkaa, hali inayomuamsha kiongozi wa mila, kwenda kushitaki kwa mkuu wa mkoa.

Chifu Mleshelwa Nzunda, amefika kwa Mkuu wa Mkoa kutoa ombi, akitaka kutiliwa mkazo uharibifu wa mazingira, akidai hali iliyopo ikiendelea, kuna shaka misitu yote itamalizika na mkoa kuingia kwenye majanga.

Anafafanua kwamba, wao wazee wa mila wapo tayari kuisaidia serikali kutumia nyoka maalum kulinda misitu kwenye maeneo yote, ili kuwadhibiti wanaoleta madhara kwenye msitu.

"Watoto wetu shuleni wanakaa chini kwa upungufu mkubwa wa madawati uliopo kwenye shule zetu," anasema Nzunda na kuendelea:

"Leo hii, miti hiyo badala ya kutumika kutengenezea madawati, watu wanakata bila utaratibu na ushauri kisha wanachomea mikaa,waturuhusu tuingize nyoka kwa ulinzi.

"Hata sisi wazee wa mila tunakosa mahala pa kufanyia matambiko, kutokana na misitu kukatwa ovyo. Tunaomba serikali itupe kibali, nyoka zilizopo katika misitu hiyo zitumike kwa ulinzi.'

**VIONGOZI WAKERWA**

Costina Kibona, Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mbozi, anaomba sheria iwachukulie hatua wananchi wanaokata kuni msituni, kwani wamekuwa wakidhalilishwa na maofisa misitu, lakini wameshindwa kuwadhibiti waharibifu wakubwa.

Cosmas Nshenye, Mkuu wa Wilaya Mbozi, anasema uharibifu wa mazingira katika wilaya hiyo umewashtua wengi, kwani kumekuwapo watu wanaovamia na kukata miti, pia kuchoma mkaa bila ya kujali kuwa ni kosa.

Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Omari Mgumba, anasema baada ya kufanya ziara katika maeneo ya misitu, ameona uharibifu mkubwa wa miti na uchomaji mkaa, akishangaa kuwapo matanuru makubwa ya mikaa.

Katika hilo, anamuagiza mtendaji wake, Katibu Tawala kuwasimamisha kazi viongozi husika; Ofisa Misitu wa Mbozi, Ofisa Tarafa wa Vwawa, pamoja na Mkuu wa kitengo cha Usafi wa Mazingira na hatua hiyo, pia ielekezwe kwa watendaji wote wanaozunguka msitu wa Namwanga, kwa kushindwa kudhibiti uharibifu huo.

Pia, Mgumba anaagiza polisi kuwasaka watu sita waliotajwa kuhusika na ukataji miti na kuwateka waandishi wa habari na viongozi wa serikali waliofika kuona uharibifu huo.

'Siwezi kukubali 'nitumbuliwe' na Rais aliyeniteua, kwa ajili ya uzembe wa viongozi wengine wanaoshindwa kusimamia majukumu yao. Nitahakikisha waharibifu wote wanakamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria," anasema Mgumba.

Ziara ya ukaguzi wa mazingira katika baadhi ya wilaya mkoani humo, iliangukia Siku ya Mazingira Duniani, ambayo kimkoa ilifanyikia wilayani Mbozi.

Mgumba anatumia nafasi hiyo kukemea baadhi ya vitendo vya wakazi wa Mbozi, wanapotajwa kuhusika na uharibifu wa mazingira na wanalipa visasi kuharibu mali za viongozi wa vijiji, kwa madai 'wamewachongea' kwa viongozi wa juu mkoani.

**VIVUTIO NA MALIASILI**

Mkuu wa Mkoa Mgumba, anasema mkoa wa Songwe umekuwa na vivutio vingi vinavyopaswa kutunzwa, ili mazingira yake yawe bora na wezeshi kuvutia watalii.

Anataja baadhi yake, ni Kimondo cha Mbozi,Unyayo na michoro ya watu wa kale kwenye kijiji cha Nkangamo wilayani Momba na Kanisa la Kale katika kijiji cha Mkulwe wilayani Momba.

Maeneo mengine ni katika kijiji cha Nanyara kilichopo Mbozi, maeneo yaliyoko wilayani Momba ni: Bwawa la Chumvi kijijini Itumbula; madaraja ya kunesa, maarufu 'vitepu tepu', Kamsamba na sehemu za kutengenezea udongo kuwa chuma zilizoko Kapele, Zaka na Ikana.

Aidha, anataja vivutio vilivyoko Momba na mlima Kwimba unaotumika kwa matambiko ya jadi, mbuga za wanyama za Lwati Songwe na jua linaloakisi mwanga Ibwembingu, pia maporomoko ya maji kwenye mto ulioko wilayani Ileje.

Vingine ni ngoma za asili Ing'oma kwa makabila ya Ileje kama vile Lipango, Ndili na Namlala.

- ***Mwandishi anapatikana kwa mawasiliano: baruapepe; yassin.ibrahimu@yahoo.com na simu + 255 766 936392 na 0718 382817.***



Mandhari ya mazingira ya Ziwa Rukwa.

AFYA

## HATUA MPYA VITA VYA UTAPIAMLO ...

# Yabuniwa mashine mpya ya kuandaa virutubishi lishe, ishara ya mapinduzi



Mhusika wa mradi wa uongezaji virutubishi kutoka asasi ya Gain, Edwin Josiah, akiweka virutubishi katika mashine kwa ajili ya kuchanganya unga wa mahindi. **PICHA: SABATO KASIKA.**

**Na Sabato Kasika**

MOJA ya ajenda muhimu nchini kukabili tatizo sugu, inajumuisha kuwapo lishe duni kwa watoto, hata wanaangukia hali ya udumavu.

Shaka iliyoko, isipoangaliwa, hali itafikia pabaya.

Serikali inaendelea kuchukua hatua, ikishirikiana na wadau wengine wanaotoa michango, nyenzo zinazoendana na miongozo ya kiserikali katika eneo hilo.

Hadi sasa, kunashuhudiwa utengenezaji wa mashine ndogo za kuweka virutubishi kwenye unga wa mahindi, ikiwa ni utekelezaji wa maagizo ya Ofisi ya Waziri Mkuu kutaka vyuo vya kiteknolojia kufanya kazi hiyo, hata kuwapa fursa wananchi wapate lishe bora.

Serikali ilishatoa maelekezo kwenye wizara hizo za kisekta kupitia taasisi zake za Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo (SIDO), Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (VETA), pia Tume ya Taifa ya Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) na wadau wengine, kutengeneza mashine za kuongeza virutubishi katika unga zitakazotumiwa na wasindikaji wadogo.

Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), imekuwa ya kwanza kutengeneza sampuli ya mashine ndogo ya kuweka virutubishi hivyo, ambayo imekaguliwa na wadau wa lishe zaidi ya wiki sasa.

Ni kazi iliyofanywa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC), shirika lisilo la kiserikali linalojishughulisha na lishe la Global Alliance for Improved Nutrition (GAIN), Child Help Tanzania (CHT),

**SAFARI NA MATARAJIO**

Meneja Mradi wa Virutubishi wa GAIN, Archad Ngemela, anasema hatua za ubunifu huo zinaenda sambamba na Mpango Jumuishi wa Lishe wa serikali wa miaka mitano unaoishia mwaka 2026.

"Mpango huo unalenga kushirikisha wazalishaji wadogo zaidi wa unga kwa kuendana na Mwongozo wa Lishe Shuleni, hivyo matarajio yetu ni kuona wabunifu zaidi wa mashine ili kumaliza utapiamlo nchini," anasema Ngemela.

Anafafanua kuwa, shirika hilo limekuwa na maelekezo ya serikali la upatikanaji chakula chenye virutubishi na kwamba hatua ya DIT kutengeneza mashine hiyo, inaonyesha jitihada za kukabiliana na ugonjwa huo zinafanyika.

Ofisa Usalama wa Chakula kutoka Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Rhoda Kidolezi, anasema lengo la serikali ni kupunguza tatizo la lishe duni nchini na anavitaka vyuo vingine kubuni mashine za aina hiyo.

"DIT wamekuwa wa kwanza kufanya ubunifu huo kwa kutekeleza maelekezo ya Ofisi ya Waziri Mkuu, hivyo ni vyema taasisi na vyuo vingine vilivyopewa maelekezo hayo, kuharakisha ubunifu wao," anasema Rhoda.

Anashauri umuhimu wa kuwapo mashine ndogo za kuongeza virutubishi katika unga, kuanzia ngazi ya chini, ambako kuna mashine nyingi za kusaga, kila moja inatakiwa kuwa na mashine ya aina hiyo.

**MAFANIKIO YALIVYO**

Selestine Mgoba, ni Ofisa Teknolojia wa Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC), anayesema mashine hiyo imekamilika kwa asilimia 80, vikibakia vichache zikiwamo matundu, ili kuzinduliwe rasmi na kuanza uzalishaji.

Anasema, ufanyaji kazi wake ni mashine hiyo inafungwa pembeni mwa eneo ambalo mahindi yanamwagwa kwenye kinu cha mashine kubwa ya kusaga na kwamba inapoanza kazi, ile yenye virutubishi inavimwaga vichanganyike na unga.

"Unajua mashine za aina hii zinazoagizwa kutoka nje zinanunuliwa kwa Sh. milioni saba kila moja, lakini za aina hii zikikamilika, zitakuwa zinauzwa kati ya Sh. milioni mbili hadi tatu," anafafanua.

**VIPI KICHWA KIKUBWA?**

Ofisa Habari wa Taasisi ya Child Help Tanzania (CHT), Militon Byemerwa, anasema kuwapo kwa mashine za kuongeza virutubishi katika unga, kunaweza kusaidia kupunguza uzazi wa watoto wa kichwa kikubwa na mgongo wazi kwa kupata lishe stahiki kwa wingi.

Anasema, chanzo kikubwa cha kuwapo watoto wenye ulemavu huo ni ukosefu wa virutubishi, hasa aina ya 'foliki asidi' kwa wajawazito, akiamini jitihada zinazoendelea zinaweza kupunguza tatizo hilo.

"Taasisi yetu inajishughulisha na huduma kwa watoto wenye ulemavu huo, hivyo tunapoona jitihada zinazofanyika za kutaka kuwapo kwa mashine nyingi za kuongeza virutubishi katika unga, tunafurahi," anasema.

Byemerwa anaeleza kuwa vyakula vinapokuwa na virutubishi na wakati huohuo, watumiaji wake wakizingatia lishe bora, inafungua mlango wa kutoweka tatizo la utapiamlo na udumavu nchini.

**MIPANGO SERIKALINI**

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Sera, Bunge na Uratibu, George Simbachawene, anasema anaahidi lishe kuwekezwa kitaifa, ikiwa ni sehemu ya mapambano dhidi ya utapiamlo, kuanzia ngazi ya kaya hadi taifa, kuhakikisha jamii inakuwa salama na kushiriki katika uzalishaji.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Sera, Bunge na Uratibu, George Simbachawene, anasema ni muhimu kuwepo jitihada za pamoja katika mapambano hayo, kwa kuwa ukosefu wa lishe una madhara makubwa kwa umma, hata kusababisha Watanzania washindwe kuzalisha kwa ufanisi.

Simbachawene, ametoa maoni hayo katika kikao kazi kilichohusisha Watendaji wa Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania (TFNC) na wadau wa maendeleo, kuhusu masuala ya lishe nchini, wiki iliyopita jijini Dodoma.

"Maeneo ya msingi ni elimu ya lishe kwa mikoa inayozalisha chakula, kwani kuna kiwango kikubwa cha utapiamlo kwa watoto," anasema Waziri Simbachawene.

Anafafanua kwamba, elimu ya lishe ya kufundishwa katika shule za msingi kuanzia darasa la kwanza hadi la saba ni jambo muhimu, ili kuwaandaa vijana kuwa mabalozi bora wa lishe hata watakapofikia hatua ya kujitegemea.

"Unapokosa lishe nzuri unapata matatizo ya afya. Kinamama wajawazito kukosa mtoto mwenye afya na mama mwenye afya nzuri, watoto huwa na udumavu wa akili na mwili. Serikali itapata hasara kwa sababu ya kuwa na watu wasio na afya bora kutokana na maradhi kwa kukosa lishe bora," anasema.



Malighafi nafaka inayotumika kuandaa lishe. **PICHA: MAKTABA.**





Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira (RUWASA), Mhandisi Clement Kivegala (kulia) na Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST), Prof. Aloys Mvuma (kushoto), wakibadilishana mikataba ya dira za maji za malipo kabla ya matumizi, baada ya kuisaini kwenye hafla iliyofanyika Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Ukomo bei huduma za maji kuanza vijijini

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imetangaza bei ukomo za huduma za maji zitakazoanza kutumika katika maeneo ya vijijini ili kuleta unafuu kwa wananchi. Bei hizo zilitangazwa jana na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA), Prof. Idrisa Mshoro, katika hafla ya kukabidhi taarifa ya utendaji ya wakala huo kwa mwaka 2020/2021.

Pia kusaini mikataba ya dira za maji za malipo kabla ya matumizi, kutangaza bei kikomo za huduma ya maji vijijini na ugawaji wa pikipiki kwa ofisi za RUWASA.

"RUWASA kupitia kikao chake cha Bodi ya Wakurugenzi kilichofanyika tarehe 25, Juni 2021 iliidhinisha bei za ukomo kwa vyombo vyote vya watoa huduma ya maji vijijini kwa kuzingatia teknolojia mbalimbali zinazotumika katika miradi ya maji vijijini baada ya kufanya tathmini ya kina ya bei zinazotozwa na vyombo vya watoa huduma ngazi ya jamii kwa sasa," alisema.

Alisema bei ya kikomo zitakazotumiwa na vyombo kwa wateja wenye dira za maji kwa miradi inayotumia nishati ya mafuta kwa uniti moja ni Sh. 2,500 na ndoo ya lita 20 itauzwa Sh. 20 na wasio kuwa na dira ya maji kwa mwezi itakuwa Sh. 15,000.

Kwa miradi ya maji inayotumia nishati ya umeme jua bei ya uniti moja itakuwa Sh.1,500 na ndoo ya lita 20 itauzwa kwa Sh. 30 na wasio na dira kwa mwezi itakuwa Sh. 7,000. "Miradi ambayo inatumia mserereko kufika kwa wateja itakuwa uniti moja ni Sh. 1,000 na ndoo ya ujazo wa lita 20 itauzwa Sh. 20 na kwa wasiokuwa na dira ya maji kwa mwezi itakuwa Sh. 5,000. "Kwa umeme wa TANESCO uniti moja itakuwa Sh. 2,000 na ndoo ya lita 20 itauzwa Sh. 40, na kwa wasiokuwa na dira kwa mwezi itakuwa 10,000," alisema.

Alisema kwa miradi inayotumia pampu za mkono, uniti moja itakuwa Sh. 1,000 na ndoo ya lita 20 itauzwa Sh. 20, wasiokuwa na dira za maji itakuwa kwa mwezi Sh. 5,000.

Kwa maji ya jumla kutoka vyanzo vikuu uniti moja ni Sh. 2,500 na ndoo ya lita 20, Sh. 50, wasiokuwa na dira za maji watalipa Sh. 15,000 kwa mwezi," alisema.

"Bei hizo zitaendana na masharti yafuatayo ikiwamo chombo chochote hakitaruhusiwa kutoza zaidi ya bei zilizoainishwa," alisisitiza.

Pia, alisema chombo chochote ambacho kinatoza bei chini ya bei kikomo kitaendelea kutoza ya awali na hakiruhusiwi kuongeza bila kupata idhini ya RUWASA.

Kadhalika, alisema chombo kinachotumia teknolojia zaidi ya moja katika uzalishaji wa maji kitatakiwa kutumia bei kikomo ya teknolojia inayochukua asilimia kubwa katika uzalishaji.

"Kufikia Juni 30, 2022 vyombo vyote vinatakiwa kuwa vimefunga dira za maji kwa wateja wake wote. Kwa wateja wa majumbani na taasisi bei zitakuwa asilimia 70 kwa kila teknolojia kama zilivyoainishwa," alisema. Vilevile, alisema bei kwa wateja wa biashara na viwanda zitabaki kama zilivyoainishwa. "Vyombo ambavyo vitashindwa kumudu gharama za uendeshaji na matengenezo ya miradi vinayosimamia kutokana na bei kikomo zilizoainishwa viwasilishe maombi ya bei maalum kwa kufuata utaratibu uliotolewa kwenye mwongozo wa upangaji bei mwaka 2020," alisema.

# NARCO yaelekezwa kujiendesha kibiashara

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, ameitaka Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO), kubadilisha mtizamo ili kujiendesha kibiashara.

Pia ameitaka kukubali kwenda na wakati kwa kutengeneza mpango wa habari, elimu na mawasiliano ili Watanzania wajue mchango wa mifugo katika maendeleo ya taifa.

Ndaki, alibainisha hayo juzi jijini hapo wakati wa uzinduzi wa Bodi ya NARCO na kuwataka wafanyakazi wa kampuni hiyo kufanya kazi kwa kuzingatia misingi ya utaalamu, uadilifu, uwajibikaji, usikivu na kuondoa mazoea.

Alisema, baada ya bodi hiyo kuanza kufanya kazi mabadiliko makubwa yanatarajiwa ili kuzalisha kampuni yenye matokeo yanayogusa wananchi. "Kaangalieni vihatarishi vinavyowakwamisha hakikisheni mnajenga kampuni inayojiendesha kwa mifumo imara ya fedha, utumishi, uchumi na kielektroniki," alisisitiza Ndaki.

Alisema pia kuna utajiri mkubwa kwenye sekta hiyo na kutaka itumike kuinua maisha ya Watanzania mchango wa Pato la Taifa.

"Sekta hii bado haijachechemuliwa vizuri, uchangiaji wake bado ni mdogo, lazima mkumbuke ranchi za taifa zinatengenezwa kutoa mchango, lakini watu huwa hawaelewi tunapozungumza Watanzania maskini tunawajumuisha na wafugaji, wanawezaje kuwa maskini? Alihoji. Kadhalika, alisema NARCO ni mkono wa serikali unaojaribu kuleta mabadiliko kwa wafugaji kupitia sekta ya mifugo na kubadili uchumi wa nchi, pia kutumika kama kichocheo cha kuondoa umaskini.

"Mkafanye biashara, zalisheni na kusambaza mbegu bora za mifugo, nyama na maziwa, bado hatuna maziwa ya kutosha, tuna lita milioni 3.1 kwa ng'ombe milioni 33.33 maziwa tunayozalisha ni kidogo sana kulingana na kiwango cha kimataifa cha lita 56 kwa mwaka kwa kila mtu," alisema.

Vilevile, aliiagiza NARCO kuanzisha wazo la kibiashara kwa wafugaji wa jadi, kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wafugaji wadogo ili kuwa na mifugo bora.

"Ninyi ni kielekezo cha ufugaji bora, Ranchi za Taifa tumezigawa kwenye maeneo madogo madogo yaani vitaru ili kuwafikia wafugaji wengi kwa wakati mmoja, hadi sasa asilimia 75 ya eneo la Ranchi iko kwenye matumizi na asilimia 25 bado inahitaji watumiaji," alisema.

Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Tixon Nzunda, alisema NARCO inahitaji mabadiliko ya mtazamo wa taasisi katika uzalishaji, mabadiliko katika mfumo uendeshaji, mabadiliko katika menejimenti ya fedha na kibiashara ili kuifanya kuwa na manufaa kwa jamii. Alisema kampuni hiyo inahitaji mambo tisa ili kubadilika ikiwa ni pamoja na mpango wa mabadiliko na rasimu ya mpango huo tayari imeshaandaliwa na imepitishwa ili kuifanya NARCO kuwa na mabadiliko.

"Kuandaa mpango wa kupata rasilimali, kubadilisha mtazamo wa fikra za utendaji kazi kwenda kwenye mawazo ya kibiashara ambapo fikra zao, mitazamo yao na wanavyofanya kazi lazima wajielekeze kwenye biashara.

"Uwazi, ni njia pekee ya kujulisha watu waelewe hayo mashamba wanayotaka kulima hayapo kwa ajili ya kulima ni kwa ajili ya mifugo tu, kutengeneza mpango wa mawasiliano kwa umma ili kuifanya kuwa taasisi inayotambulika kwa umma inafanya nini ikiwa ni pamoja na kufanya kazi kwa kuzingatia misingi ya utaalamu na bodi ielekeze menejimenti ifanye kazi kwa misingi ya uwajibikaji," alisema.

# Kiwanda cha mbolea kuanza uzalishaji Julai

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KIWANDA cha mbolea cha Itracom, Nala jijini hapa, kitaanza uzalishaji wa tani 200,000 mwezi Julai mwaka huu huku utafiti ukibainisha ubora wa mbolea hiyo.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alibainisha hayo juzi alipofanya ziara ya kutembelea kiwanda hicho kujionea maendeleo ya ujenzi.

Alisema kiwanda hicho kitaanza kwa kuzalisha tani 200,000 za mbolea aina Organo Mineral, Branding na Lime ambayo itatumika kwenye msimu huu wa kilimo.

Alisema utafiti uliofanywa na wizara hiyo kupitia vituo vyake vya utafiti umebaini mbolea hizo zinafaa kwenye kilimo cha mahindi, maharage, mpunga na mtama.

"Hizi tani 200,000 ni uzalishaji wa awali, lakini kiwanda kina uwezo wa kuzalisha tani 600,000 kwa mwaka ambazo ni mahitaji halisi ya mbolea nchini," alisema.

Alisema utafiti huo umefanyika katika mikoa ya Katavi na Rukwa kwenye mazao hayo na kuonyesha matokeo chanya.

"Hii mbolea inayozalishwa kiwandani hapa ni nzuri na itasaidia kupunguza hasara wanayopata wakulima kwa kutumia mbolea zenye kemikali ambayo haiendani na udongo uliopo," alisema Bashe.

Kutokana na hilo alisema baada ya kubaini mbolea hiyo inafaa katika ardhi ya Tanzania, serikali imeahidi kusaidia ili Julai uzalishaji uanze kwa ajili ya msimu ujao wa kilimo.

"Serikali itatoa ruzuku kwa mara ya kwanza katika kiwanda cha ndani na tunafanya hivi ili kutengeneza ajira za ndani kwa vijana," alisema Bashe.

Hata hivyo, Waziri Bashe alisema serikali inatarajia kukutana na uongozi wa kiwanda cha Minjingu ili kujadiliana kuingia mkataba wa kuuziana malighafi na Itracom ili wawapatie malighafi zinazokosekana kiwandani hapo kwa ajili ya uzalishaji mbolea.

Alisema tayari serikali imewaongezea hekta 23 kwa ajili ya upanuzi wa kiwanda hicho.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Itracom, Nduwimana Nazaire, alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuruhusu uwekezaji ili kukuza uchumi wa Tanzania.

"Tunatarajia ifikapo mwaka 2024 kuzalisha tani milioni 1.5 za mbolea hapa nchini ambazo zitauzwa na nje ya nchi," alisema.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, alisema wanashirikiana na kiwanda hicho ili uzalishaji uanze Julai, mwaka huu kama walivyokubaliana.





# Bashe kufungua maonyesho Nanenane

Na Nebart Msokwa,

MBEYA

WAZIRI wa Kilimo, Husein Bashe anatarajiwa kuwa mgeni rasmi kwenye uzinduzi wa Maonyesho ya Wakulima (Nanenane) kitaifa ambayo yanafanyika mkoani hapo kuanzia Agosti 1 - 8, mwaka huu.

Maonyesho hayo yanatarajiwa kufungwa na mmojawapo wa viongozi wakubwa wa kitaifa ambaye bado hajawekwa wazi.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliyasema hayo jana jijini Mbeya alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu maandalizi ya maonyesho hayo ambapo alisema mpaka sasa maandalizi hayo yamefikia zaidi ya asilimia 80.

Homera alisema maandalizi ya maonyesho hayo yanafanywa kwa ushirikiano kati ya mikoa yote ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Wizara ya Kilimo na waonyeshaji mbalimbali wa sekta za kilimo na mifugo watashiriki kutoka ndani na nje ya Tanzania.

Alisema mpaka sasa wamewaalika waonyeshaji kutoka katika mikoa mbalimbali ya nchi jirani zinazopakana na Tanzania zikiwamo za Afrika Mashariki na za Ukanda wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Aliyataja mataifa yatakayoshiriki kuwa ni pamoja na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Zambia, Malawi, Msumbiji, Rwanda, Burundi, Uganda na Kenya.

"Kwanza tunamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kurejesha maonyesho haya, pili tunamshukuru kwa kuridhia kitaifa yafanyikie mkoani kwetu Mbeya katika Uwanja wa John Mwakangale na tatu tunawaalika wakulima, wafugaji na wavuvi nchini kote kuja kuonyesha vitu vyao," alisema Homera.

Alisema maonyesho ya mwaka huu ni tofauti na yaliyokuwa yanafanyika miaka iliyopita kwa maelezo kuwa mwaka huu hakutakuwa na maonyesho katika Kanda yoyote zaidi ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

# Serikali yaanza utekelezaji uoto wa asili

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, Idara ya Mazingira, imeanza utekelezaji wa mradi wa kurejesha uoto wa asili wa maeneo ambayo yameathiriwa na shughuli za kibinadamu katika mikoa mitano ya Nyanda za Juu Kusini wenye thamani ya zaidi ya Dola za Kimarekani milioni 75.

Mkurugenzi Msaidizi kutoka Idara ya Mazingira katika Ofisi ya Makamu wa Rais, Faraja Ngalageza, aliyasema hayo jana jijini hapo wakati akizungumza na watendaji kutoka kwenye halmashauri ambazo mradi huo utatekelezwa.

Ngalageza aliitaja mikoa ambayo mradi huo utatekelezwa katika mikoa ya Mbeya, Rukwa, Katavi, Njombe na Iringa ili kurejesha uoto wa asili ambao umeharibiwa kutokana na shughuli za kibinadamu na kutunza vyanzo vya maji vya mabonde mawili yanayopatikana kwenye mikoa hiyo.

"Lengo kubwa la mradi huu ni kulinda vyanzo vya maji vya Bonde la Ziwa Rukwa, lakini Bonde la Rufiji ambako kwa ukanda huu linahusisha Mto Ruaha Mkuu, ambao ni muhimu sana kwa ikolojia ya wanyama na hata uzalishaji wa umeme nchini," alisema Ngalageza.

Alisema halmashauri zitakazohusishwa kwenye mradi huo ni zinazoguswa na mabonde hayo mawili.

Kwa upande wake, Mratibu wa mradi huo kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais, Dk. Damas Mapunda, alisema mradi huo umepata fedha zaidi ya Dola za Marekani mil. 11.285 kutoka mfuko wa mazingira wa dunia.

"Lakini mradi huu utatumia fedha za ndani kutoka taasisi za kisekta na halmashauri ambazo zinajumuishwa kwenye mradi na kufanya thamani ya mradi mzima kuwa Dola za Marekani milioni 75.5," alisema Mapunda.

Alisema mradi huo utakuwa na manufaa makubwa kwa taifa kwa vile utasaidia kuyafanya mazingira kuwa rafiki kwa shughuli za kiuchumi kama vile kilimo, utalii na pia kufanikisha miradi mikubwa ya uzalishaji umeme inayopatikana kwenye Bonde la Mto Ruaha Mkuu na Rufiji.

Mwakilishi wa Katibu Tawala Mkoa wa Mbeya, Said Madito, alisema ili mradi huo uwe na tija ni muhimu wananchi washirikishwe kulinda mazingira yasiharibike.

"Naamini kuwa wananchi wakishirikishwa na kuelewa vizuri dhana ya mradi huu, watakuwa mabalozi wa utunzaji wa mazingira na hivyo watawezesha mradi kufanikiwa kwa kiwango kikubwa, rai yangu ni kutaka katika maeneo yote ya mradi, wananchi wasiachwe nyuma, washirikishwe," alisema Madito.

Pia, mradi huo unapaswa kuwa endelevu na ili liwezekane wananchi wakauelewa na kuelimishwa kuhusu umuhimu wa utunzaji wa mazingira.

Baadhi ya wadau wa mazingira walisema kuwa endapo mradi huo utafanikiwa utakuwa na faida kubwa kuanzia kwenye jamii mpaka serikalini kwa vile unagusa maeneo muhimu ya uchumi.

Maximilian Kempanju, mdau wa mazingira mkoani Mbeya alisema kuwa faida za mradi huo ni kubwa kutokana na kujikita kutunza mazingira ambayo ni kichocheo kikubwa cha upatikanaji wa mvua kwenye maeneo hayo.

"Upatikanaji wa mvua za uhakika ni kichocheo kikubwa cha shughuli nyingi za kiuchumi, tena kuanzia zile zinazowagusa wananchi wa chini yaani kilimo mpaka shughuli kubwa za kichumi kama vile upatikanaji wa umeme viwandani, hivyo mradi huu utakuwa ni neema kwa taifa," alisema Kempanju.

Aliiomba serikali kujenga misingi endelevu ambayo hata baada ya miaka mitano ya utekelezaji wa mradi huo kumalizika, utunzaji wa mazingira uendelee kwa manufaa ya jamii na taifa kwa ujumla.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, akizungumza na waandishi wa habari jana kuhusu utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ndani ya mkoa huo, ikiwamo ukusanyaji wa mapato, mpaka sasa umefikia asilimia 101. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mbeya yavuka lengo ukusanyaji mapato

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya imesema imevuka lengo la ukusanyaji wa mapato kwa kufikia zaidi ya asilimia 101 ya malengo ambayo iliwekewa na Serikali Kuu huku halmashauri zake zote zikitarajiwa kufikia asilimia 100 kabla ya Julai mosi mwaka huu.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera aliyasema hayo jana alipozungumza na vyombo vya habari kuhusu utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo ndani ya mkoa huo ikiwamo ukusanyaji wa mapato.

Alisema katika mwaka wa fedha 2021/2022, mkoa huo ulipangiwa na Serikali Kuu kukusanya Sh. bilioni 42.6, lakini mpaka sasa umekusanya Sh. bilioni 43.1 sawa na asilimia 101.

Alisema katika makusanyo hayo mapato Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ndiyo yanayoongoza kutokana na kupewa lengo la kukusanya Sh. bilioni 4.3 na kufikia Juni 21, ilikusanya Sh. 5,000,000,000 sawa na asilimia 117.

Aliitaja halmashauri ya pili kuwa ni Chunya ambayo ilipangiwa kukusanya Sh. bilioni 4.8, mpaka sasa imekusanya Sh. 5,000,000,000 sawa na asilimia 104, ikifuatiwa na Jiji la Mbeya ambalo lilipangiwa kukusanya Sh. bilioni 16.6 na kukusanya Sh. bilioni 16.7 sawa na asilimia 101.

Halmashauri ya nne kuwa ni Busokelo ambayo ilipangiwa kukusanya Sh. bilioni 1.59 na imekusanya Sh. bilioni 1.59 sawa na asilimia 100.

Halmashauri zingine tatu bado hazijafikisha asilimia 100, lakini zina wastani mzuri na mpaka kufikia mwisho wa mwaka wa fedha zitakuwa zimekamilisha ukusanyaji huo.

Halmashauri hizo ni Kyela ambayo ilipangiwa kukusanya Sh. bilioni 3.8, iliyokusanya Sh. bilioni 3.7 sawa na asilimia 97, Halmashauri ya Rungwe ilipangiwa kukusanya Sh. bilioni 5.3 na kukusanya Sh. bilioni 5.1 sawa na asilimia 96.

Halmashauri ya Mbarali ilipangiwa kukusanya Sh. 5,000,000,000, lakini mpaka kufikia Januari ilikuwa imefikia asilimia 100 na tuliamua kuiongezea malengo na kuitaka ikusanye Sh. bilioni 6.1 na mpaka sasa wamefikia asilimia 95 hatua ambayo ni nzuri sana," alisema Homera.

Aliwataka wakurugenzi wa halmashauri ambazo bado hazijafikisha asilimia 100 kuhakikisha zinakamilisha kabla ya Juni 30, mwaka huu ili kuendana na zingine.

Vilevile, alisema mkoa huo unakusudia kutoa tuzo maalumu kwa wakurugenzi na wakuu wa wilaya ambazo zimefanya vizuri kwenye makusanyo hayo ili kuwa chachu kwa miaka ijayo ya fedha.



# Waandishi wa habari watakiwa kufahamu sheria

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIBU Mtendaji wa Tume ya Utangazaji Zanzibar, Suleiman Abdallah, amewataka waandishi wa habari kusoma masuala ya sheria ili kuzifahamu katika kutekeleza majukumu yao.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua mafunzo ya sheria kwa waandishi wa habari mjini hapo, yaliyoandaliwa na Baraza la Habari Tanzania (MCT).

Aliwataka waandishi wa habari kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia sheria na misingi ya taaluma huku wakiongozwa na maadili ya habari ili vyombo vya habari vitumike kujenga umoja, kuimarisha demokrasia na kukuza utawala bora. "Nguvu ya vyombo vya habari itumike kujenga na sio kubomoa, kuimarisha na kujiepusha na kauli za chuki na badala yake wajikite kuibua kero za wananchi na kutoa sauti kwa wasio na sauti pamoja na kuzingatia makundi ya pembezoni," alisema.

Pia mafunzo hayo ni dira ya kutoa mwanga kwa waandishi wa habari kuzifahamu kwa kina sheria ili kujenga hoja madhubuti kwa kutumia kalamu zao na Wizara ya Habari itaendelea kushirikiana na wadau katika kuimarisha kada ya habari ikiwamo kuwa na sheria bora.

Alisema kuwa masuala ya sheria ni muhimu katika kuendeleza kada ya habari nchini kutokana na umuhimu wa kada hiyo kukuza na kuimarisha demokrasia ya kweli pamoja na uwazi na uwajibikaji kwa viongozi.

"Mafunzo haya ni muhimu kuyazingatia ili waandishi tuwe mabalozi wazuri kufanya utafiti wa kina wa sheria hizi za habari, kujua wenzetu wapo wapi katika maendeleo ya sheria nzuri za habari ili nasi tuwe mfano wa kuiga wakati wa kufanya uchambuzi wa kina," alisema Abdallah.

Naye Katibu Mtendaji wa MCT, Kajubi Mukajanga, alisema kuwa kuzisoma sheria za uandishi wa habari ni muhimu ili kuondoa changamoto zinazojitokeza katika kazi zao.

"Bila habari hakuna maendeleo hivyo tuendelee kupeana ushirikiano ili kupeleka mbele dau la habari," alisema Kajubi.

Akitoa mada kuhusu haki ya kupata habari, Wakili Mpale Mpoki, alisema kila mtu anayo haki ya kupewa taarifa na wakati wote kuhusu matukio mbalimbali yanayotokea duniani ambayo ni muhimu kwa maisha ya wananchi.

"Uhuru wa kutoa maoni ni haki ya msingi katika kuleta maendeleo kutafuta ukweli kuimarisha demokrasia na utawala bora," alisema Mpoki.

Kwa upande wake Mdhamini wa Baraza la Habari Ofisi za Zanzibar, Shifaa Said Hassan, alisema nyanja ya habari ni kupeana ushirikiano wa kukuza taaluma




Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya (kushoto), akiwaongoza maofisa waandamizi pamoja na wafanyakazi wa Shirika la Bima Zanzibar (ZIC) kukabidhi msaada wa vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. mil. 30 kwa uongozi wa Hospitali ya Rufani ya Mnazi Mmoja iliyoko visiwani humo, ikiwa ni maadhimisho ya 53 tangu kuanzishwa kwa shirika hilo. Kulia ni Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali ya Mnazi Mmoja, Dk. Marijani Msafiri, Mkurugenzi wa Bima ya Kawaida wa ZIC, Jape Khamis (katikati) na Mwenyekiti wa Bodi ya ZIC, Ramadhani Mwalimu Khamis. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mnazi Mmoja yakabidhiwa vifaa tiba vya milioni 30/-

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Saada Mkuya, amewaongoza maofisa waandamizi pamoja na wafanyakazi wa Shirika la Bima Zanzibar (ZIC), kukabidhi msaada wa vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. milioni 30 katika Hospitali ya Rufani Mnazi Mmoja ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya 53 tangu kuanzishwa kwa shirika hilo.

Vifaa hivyo ni pamoja na taa inayosaidia wakati wa upasuaji, kifaa cha uangalizi wa wagonjwa wa dharura pamoja na mashine za kupima shinikizo la damu.

Tukio hilo lilipambwa na maandamano ya amani yaliyoongozwa na waziri huyo kutoka makao makuu ya Shirika hilo hadi Hospitali ya Mnazi Mmoja na kurudi kwenye ofisi ya makao makuu ya shirika hilo.

Akizungumza wakati wa hafla fupi ya makabidhiano hayo iliyofanyika kwenye viunga vya hospitali hiyo, Dk. Saada pamoja na kulipongeza shirika hilo linalomilikiwa kwa asilimia mia moja na Serikali ya Zanzibar (SMZ), alisema msaada huo ni uthibitisho tosha kuwa shirika hilo linajiendesha kwa faida huku likitimiza vyema malengo ya kuanzishwa kwake.

"Pamoja na kutumia maadhimisho haya kujiweka karibu zaidi na wateja wenu, nimefurahishwa zaidi kuona kwamba mmeamua kutenga sehemu ya faida yenu ili kuokoa maisha ya Watanzania wenzetu wanaopigania afya zao hospitalini.

Hii imekuwa ni moja ya sababu iliyonisukuma kuungana nanyi hii leo...hongereni sana ZIC kwa kuwa mngeweza tu kujipongeza wenyewe ila mkaona ni vyema mlichokipata mkirejeshe kwa jamii kupitia jambo hili muhimu," alisema.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika hilo, Ramadhani Mwalimu Khamis, alisema hatua hiyo ni sehemu ya kuunga mkono juhudi za serikali pamoja na wadau mbalimbali wakiwamo wateja wa shirika hilo katika kuboresha sekta ya afya hapa nchini.

"Shirika la Bima Zanzibar tunaamini kupitia wananchi hawa, ndipo biashara yetu inapofanikiwa, tuna wajibu wa kuchangia maendeleo ya nchi hii kupitia nyanja mbalimbali ikiwamo sekta ya afya. Changamoto za sekta ya afya kwetu ni jambo la kipaumbele, kwa kuwa afya ndio msingi wa uchumi na uzalishaji mali na ni kichocheo kikuu cha maendeleo ya wananchi," alisema.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Bima ya Kawaida wa ZIC, Jape Khamis, alisema kupitia maadhimisho hayo shirika hilo limekuwa karibu zaidi na wadau wake muhimu wakiwamo wateja pamoja na msaada huo shirika hilo pia limetoa zawadi mbalimbali za papo kwa papo kwa wateja.

"Katika tukio lingine kubwa ambalo ndiyo litahitimisha kilele cha maadhimisho haya, tumeandaa hafla maalum tukilenga kukutana na wateja wetu kujipongeza kwa pamoja, kupata mrejesho kutoka kwa wateja kuhusu huduma zetu, kujadili fursa za biashara pamoja na kuzindua programu maalum ya mtandaoni kwa ajili ya huduma za shirika yaani Online Application," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali ya Mnazi Mmoja, Dk. Marijani Msafiri, alisema msaada huo utaongeza tija zaidi katika utoaji wa huduma za kiafya hospitalini hapo kutokana na uhaba wa vifaa hivyo huku pia baadhi ya vifaa vikiwa vinakabiliwa na changamoto ya uchakavu.

"Miongoni mwa vifaa hivi ni pamoja na taa zinazosaidia upasuaji ambazo kiukweli zinapatikana kwa shida hivyo kupitia msaada huu tutaokoa maisha ya wananchi wengi. Zaidi pia tunashukuru kwa msaada wa vifaa vya uangalizi wa wagonjwa wa dharura husussani wale changamoto ya COVID-19 kwa kuwa mashine hii ni muhimu katika kuonyesha kiasi cha hewa ya Oxygen kilichoko kwenye mapafu ya mgonjwa," alisema.

## Wawakilishi wapitisha bajeti ya serikali 2022/23

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi wamepitisha bajeti ya serikali kwa mwaka wa fedha 2022-2023 na kuidhinisha Mswada wa matumizi ya fedha hizo Sh. trilioni 2.59 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Miradi hiyo imejikita katika kujenga miundombinu pamoja na uchumi wa buluu katika ujenzi wa viwanda.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya akizungumza katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani alisema kitendo cha wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kupitisha muswada wa sheria ya kuidhinisha makisio ya matumizi ya Sh. trilioni 2.59 unakwenda kuiruhusu serikali kuanza kutekeleza malengo yake kwa mwaka wa fedha 2022-2023.

Dk. Mkuya alisema bajeti ya serikali kwa mwaka wa fedha 2022-2023 imejikita katika kuimarisha miundombinu ya barabara pamoja na ujenzi wa viwanda vya mazao ya baharini na kutegemea kutoa ajira zipatazo 200,000 kwa wananchi.

Alisema serikali imetenga fedha Wizara ya Uvuvi na Uchumi wa Buluu, Sh. bilioni 36 kwa ajili ya kuwanufaisha wajasiriamali ikiwamo wa mazao ya baharini na wanawake kwa asilimia 54 watanufaika.

Alisema wakulima wa kilimo cha mwani wamelengwa na kupewa kipaumbele cha kwanza na jumla ya boti 500 zinatarajiwa kutengenezwa na kugaiwa kwa wakulima kuwawezesha kufika katika kina kikubwa cha maji.

"Bajeti hii imewalenga wajasiriamali wanawake kuona kwamba wanapiga hatua kubwa ya maendeleo ikiwamo kufaidika na mazao ya baharini na kilimo cha mwani pamoja na majongoo ya baharini na ufugaji wa samaki," alisema.

Alisema katika bajeti ya mwaka 2022-2023, ujenzi wa miundombinu ya barabara zinazokwenda vijijini zimepewa kipaumbele cha kwanza ikiwamo kwa upande wa Pemba barabara za Wete hadi Chakechake yenye urefu wa kilomita 22.1 inatarajiwa kujengwa.

Alifahamisha fedha za ujenzi wa barabara hiyo zipo tayari zimetengwa ambazo zinakwenda kuiunganisha mikoa miwili ya kisiwa cha Pemba kiuchumi na uwekezaji ikiwamo katika maeneo huru ya kiuchumi ya Micheweni.

"Mikakati ya bajeti hii tumesema inakwenda kukifungua kisiwa cha Pemba miundombinu ya barabara pamoja na ujenzi wa bandari tatu pamoja na uwanja wa ndege wa Pemba...fedha za utekelezaji wa miradi hiyo zipo," alisema.

Kwa upande wao baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, wakichangia bajeti hiyo walifurahishwa na mikakati iliyowekwa ambayo imelenga kujenga miundombinu na kukifungua kisiwa hicho kiuchumi na uwekezaji.

Mwakilishi wa Jimbo la Ziwani, Suleiman Makame, alisema anaunga mkono bajeti hiyo ambayo inakwenda kukitangaza kisiwa cha Pemba kwa kujenga miundombinu ya barabara na bandari ili kukiunganisha kisiwa cha Pemba na nchi jirani ya Kenya.

HABARI KIMATAIFA

# Rais Ukraine akata tamaa, asema hali inakuwa ngumu

**KYIV,** UKRAINE

RAIS wa Ukraine, Volodymymry Zelensky, amesema hali imekuwa ngumu katika jimbo la Luhansk kwa sasa wakati mapigano yakizidi kushika kasi.

Akizungumza katika hotuba yake ya kila siku, kiongozi huyo alisema eneo la mapigano hakuna kilichobadilika, hata hivyo wanajeshi wake wanajitahidi kuimarisha ulinzi.

"Kusema ukweli hali ni ngumu pale Luhansk kwa sasa, wavamizi wanaweka shinikizo kubwa kuelekea Donetsk," alisema Zelensky.

Kulingana na kiongozi huyo katika jimbo la Kharkiv, vikosi vya Russia vinashambulia kwa makombora mengi.

"Wamejitahidi kwa kila njia yoyote kuwazuwia wavamizi, lakini jeshi la Russia halielewi chochote. Linafanya uharibifu tu, kwa njia hii inaonyesha makamanda wake hawana msimamo," aliongeza kiongozi huyo.

**15 WAUAWA MASHAMBULIZI YA MAKOMBORA KHARKIV**

Wanajeshi wa Russia wameupiga mji wa pili kwa ukubwa nchini Ukraine, Kharkiv na maeneo jirani kwa kutumia makombora na kuwaua watu 15.

Ukraine ilisema mashambulizi hayo ni jaribio la kuilazimu kuondoa zana zake za kivita pamoja na wanajeshi kutoka uwanja wa mapambano.

Mashambulizi hayo ya Russia mjini Kharkiv, yaliyoanza juzi hadi asubuhi ya jana yaliongezeka maradufu kiasi ambacho kiliongeza hofu katika eneo hilo ambalo maisha ya kawaida yalikuwa yanarejea tangu Ukraine ilipowarudisha nyuma wanajeshi wa Russia.

Rais wa Ukraine, Volodymyr zelenskiy, alitoa wito kwa Umoja wa Ulaya kuiwekea vikwazo zaidi Russia wakati mapigano bado ni makali katika eneo la Donbas.

Iwapo Umoja wa Ulaya utaweka vikwazo hivyo, basi huu utakuwa ni mzunguko wa saba wa vikwazo ambavyo Russia imewekewa lakini inaonekana kutotetereka kiuchumi.

Ripoti ya uongozi wa operesheni za vita nchini humo, ilieleza kisiwa cha Nyoka kilichoko katika bahari nyeusi kimepigwa kwa makombora.

Kulingana na ripoti hiyo, mfumo wa kukinga mashambulio ya anga aina ya Pantsir S1, kituo cha uongozaji wa safari za ndege na zana nyingine za kijeshi vilivyoko kwenye kisiwa hicho vilisambaratishwa kwa kombora.

"Ukusanyaji wa taarifa kamili kuhusu shambulio hilo unaendelea," ulisema ujumbe huo uliotumwa kwenye ukurasa wa Facebook.

Russia ilithibitisha juzi kuwa eneo hilo la kisiwa cha Nyoka au linajulikana kama Zmeiny, lilipigwa kwa makombora yake.

Wizara ya Ulinzi ilisema vikosi vya Russia viliharibu silaha za adui vilipofyatua makombora yake katika Kisiwa cha Nyoka na hakuna hata moja wao aliyelenga shabaha.

Februari 24, jeshi la Russia lilishambulia eneo la Ukraine na udhibiti wa kisiwa cha Zmeiny katika Bahari Nyeusi, kilomita 140 kutoka Odessa.

**WAZIRI LAVROV AELEKEA IRAN KWA MAZUNGUMZO**

Waziri wa Mambo ya Nje wa Russia, Sergei Lavrov, amefanya ziara nchini Iran kwa mazungumzo ya kuimarisha ushirikiano wa kibiashara na nishati.

Nchi hizo mbili zinakabiliana na vikwazo vya kiuchumi vya nchi za Magharibi.

Iran na Russia zina hifadhi kubwa za mafuta na gesi lakini zimebanwa na vikwazo ambavyo vinazuia uwezo wao wa kuuza bidhaa hizo nje ya nchi.

Shirika rasmi la habari la Iran IRNA lilisema Lavrov atakutana leo na waziri mwenzake Hossein Amir-Abdollahian.

Russia iliwekewa vikwazo kufuatia uvamizi wake wa Februari wa nchi jirani Ukraine, wakati uchumi wa Iran umekuwa ukiathirika chini ya vikwazo vikali vilivyowekwa upya na Marekani mwaka wa 2018, kufuatia kujiondoa kwa marekani katika makubaliano ya nyuklia kati ya Iran na mataifa yenye nguvu.

**DW**

# Rais Chakwera amvua madaraka makamu wake

**LILONGWE,** MALAWI

RAIS wa Malawi, Lazarus Chakwera, amemvua madaraka yote makamu wake, Saulos Chilima, baada ya kiongozi huyo kukumbwa na kashfa ya ufisadi ya dola milioni 150 sawa na shilingi bil. 349.7

Ripoti ya Taasisi ya Kupambana na Rushwa nchini humo (ACB) iliwataja maofisa 53 wa sasa na wa zamani kuwa walipokea pesa kwa mfanyabiashara kutoka Uingereza na Malawi, Zuneth Sattar kati ya 2017 na 2021 kwa lengo la kumpendelea katika kandarasi za serikali.

Hata hivyo, makamu huyo wa rais amekanusha tuhuma hizo, lakini hajasema chochote kuhusu hatua hiyo iliyochukuliwa na rais.

Tuhuma hizo zinatokana na kandarasi 16 ambazo zinahusisha kutoa huduma kwa Polisi na Jeshi la Ulinzi la nchi hiyo zilizopewa kampuni tano za Sattar.

Maofisa waliotajwa kwenye ripoti hiyo ni pamoja na makamu huyo wa rais na mkuu wa polisi ambaye amefukuzwa kazi.

Hata hivyo, sheria ya Malawi hairuhusu rais kumfukuza kazi au kumsimamisha kazi makamu wake kwa vile huyo ni kiongozi aliyechaguliwa.

"Kila ninachoweza kufanya kwa sasa, ambacho nimeamua kufanya, ni kunyima ofisi yake majukumu yoyote aliyokabidhiwa huku nikisubiri ofisi ithibitishe madai dhidi yake," alisema rais katika hotuba kwa taifa hilo juzi.

Chakwera aliungana na Chilima kumshinda Peter Mutharika katika uchaguzi wa urais wa 2020.

Wawili hao walikuwa wameahidi kupambana na ufisadi serikalini. **BBC**



Watalii wakifurahia kutazama kile kiitwacho 'Usiku Mweupe', katika kituo cha kihistoria cha mji wa St. Petersburg jana, tukio hilo huvutia maelfu ya watalii wanaotembelea nchi ya Russia. **PICHA: EPA**

# Tetemeko la ardhi laua 920 Afghanistan

**KABUL,** AFGHANISTAN

TETEMEKO kubwa la ardhi limeikumba Afghanistan na kusababisha watu 920 kupoteza maisha na mamia wengine kujeruhiwa.

Picha za angani zinaonyesha maporomoko ya ardhi na nyumba zilizoharibiwa zilizojengwa kwa udongo mashariki mwa mkoa wa Paktika, ambapo waokoaji wanahangaika kuwatafuta watu waliofukiwa na vifusi. Katika maeneo ya mbali, helikopta zilionekana zikitumika kuwasafirisha watu walioathirika na kuwapeleka hospitalini.

Kiongozi wa Taliban, Hibatullah Akhundzada, alisema mamia ya nyumba ziliharibiwa na huenda idadi ya waliofariki na kujeruhiwa itaongezeka.

Naibu Waziri Usimamizi wa Majanga, Sharafuddin Muslim, aliuambia mkutano wa wanahabari kuwa takriban watu 920 wameuawa na wengine 600 kujeruhiwa.

Tetemeko hilo lilipiga takriban kilomita 44, kutoka mji wa kusini-mashariki wa Khost muda mfupi baada ya saa 1:30 usiku wakati watu wengi walikuwa wamelala majumbani mwao.

Matetemeko ya ardhi yanasababisha uharibifu mkubwa nchini Afghanistan, ambako kuna maeneo mengi ya vijijini yamejengwa kiholela.

Maofisa wa Taliban walitoa wito kwa mashirika ya misaada kukimbilia katika maeneo yaliyoathiriwa mashariki mwa taifa hilo.

Miongo kadhaa ya migogoro imefanya kuwa vigumu kwa nchi hiyo maskini kuboresha ulinzi wake dhidi ya matetemeko ya ardhi na majanga mengine ya asili, licha ya jitihada za mashirika ya misaada ya kuimarisha baadhi ya majengo kwa miaka mingi.

Hata kabla ya Taliban kuchukua madaraka, huduma za dharura za Afghanistan ni adimu sana na haziwezi kukabiliana na majanga ya asili kikamilifu na ina ndege chache za uokoaji. **BBC**

# KOCHA CHELSEA ATUA Z'BAR

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

WANAMICHEZO mbalimbali wameanza kuwasili Zanzibar kuelekea Kongamano la Michezo la Mpira wa Miguu (Tanzania Football Sumit -TFS), linalotarajiwa kufanyika visiwani hapo Jumamosi na Jumapili wiki hii.

Miongoni mwa waliowasili ni pamoja na Kocha wa zamani wa Klabu ya Chelsea ya England, Avram Grant na baadhi ya mawakala wa wachezaji kutoka nchi mbalimbali.

**Akizungumza na gazeti hili jana kuhusu kongamano hilo, Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Afri Soccer, Petter Siamon, alisema tayari wageni kutoka nchi mbalimbali wameanza kuwasili kwa ajili ya kahudhuria kongamano hilo.**

Alisema maandalizi kuelekea kongamano hilo la TFS, yanaendelea kufanyika sambamba na kuwapokea wageni wanaowasili na shughuli nyingine zinazohusisha kongamano hilo ikiwamo kutafuta vipaji kwa wachezaji wanaocheza soka.

Alisema lengo kubwa la kongamano hilo ni kuwaleta pamoja wadau wa michezo hasa wa mpira wa miguu, kubadilishana mawazo kuona kwa kiasi gani soka la Afrika linaendelea kupiga hatua.

Kwa upande wa Kocha wa zamani wa Chelsea, Grant akizungumza na waandishi wa habari baada ya kuwasili Zanzibar, alisema amefurahi kupata mwaliko wa kuhudhuria kongamano hilo pamoja na kuwa visiwani hapo.

Alisema anamatumaini makubwa kongamano hilo litaleta fursa kwa wanamichezo kushirikiana na kubadilishana mawazo juu ya maendeleo ya Soka la Afrika na duniani kwa ujumla. Kongamano hilo limeandaliwa na Taasisi ya Afri Soccer kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Zanzibar pamoja na Shirikisho la Mpira wa Miguu Zanzibar, ZFF.




Watengenezaji, watangazaji na washawishi wa vipindi pendwa vya Maisha Magic Poa wakiwa pamoja na Mkuu wa Kitengo cha Masoko wa Dstv Tanzania, Ronald Baraka Shelukindo, katika hafla fupi ya uzinduzi wa msimu mpya wa vipindi vya Maisha Magic Poa chaneli 144 ndani ya DStv, jijini Dar es Salaam juzi. **MPIGAPICHA WETU**

# *Maisha Magic Poa yazindua 'Usichukulie Poa Vitu vya Poa'*

**Na Mwandishi Wetu**

MAMBO yanazidi kunoga ndani ya chaneli maarufu ya Maisha Magic Poa ndani ya DStv ambapo imezindua rasmi msimu mpya wa vipindi vyake kabambe vya Watubaki, Original Comedy, Ya Walimwengu, Salama pamoja na Maskani Poa.

Msimu huu mpya umeboreshwa zaidi huku kipindi cha 'Maskani Poa' kikiwa na watangazaji wapya ambao ni msanii maarufu Shilole (Zuena Mohammed) na mtangazaji nguli Baba Levo (Clyton Chipando), ambao wanaleta chachu mpya katika kipindi hicho msimu huu wa pili. Akizungumza jijini Dar es Salaam juzi wakati wa hafla fupi ya kuzindua kampeni ya msimu mpya wa vipindi hivyo, iliyopewa jina la 'Usichukulie Poa Vitu vya Poa', Mkuu wa Masoko wa DStv Tanzania, Baraka Shelukindo, alisema msimu huu wa pili umezingatia sana maoni ya watazamaji kuhusu vipindi hivyo na wanaamini kuwa watazamaji watavifurahia zaidi.

"Wakati wote tunazingatia sana maoni ya watazamaji wetu, ndiyo sababu katika msimu huu mpya mtashuhudia mabadiliko kadhaa katika vipindi hivi na yote hii tunafanya ili kuhakikisha kuwa mtazamaji wetu anapata kile anachopenda," alisema Shelukindo na kubainisha kuwa moja ya mabadiliko yaliyofanywa ni pamoja na kuwa na watangazaji wapya wa kipindi cha Maskani Poa ambapo sasa kitakuwa na Shilole na Baba Levo.

"Wale wapenzi wa vichekesho wajiandae vema kwani mbavu zao zitakuwa na wakati mgumu sana katika msimu huu mpya wa vichekesho vya Original Comedy na Watubaki."

Alisema wakali wa vichekesho wakiwamo Masanja Mkandamizaji, Mpoki na Wakuvanga kutoka Original Comedy, wameahidi kuwavunja mbavu watazamaji wa kipindi chao kinachoruka kila siku ya Jumapili saa 2:00 usiku katika chaneli ya Maisha Magic Poa – DStv 144 inayopatikana katika kifurushi cha DStv Poa kwa Sh. 9,900.

"Wachekeshaji maarufu – Watubaki, wao wamesema hawatavunja mbavu za watazamaji, bali msimu huu watazichana kabisa, kikundi hicho kinachojumuisha wachekeshaji maarufu kama Deo, Mzee Shayo na Kipotoshi, kimekuwa gumzo kwa kumwaga vimbwanga na vichekesho kabambe katika kipindi cha Watubaki kinachurushwa Maisha Magic Poa DStv 144 ndani ya kifurushi cha DStv Poa cha Sh. 9,900, bila shaka msimu huu utakuwa ni moto zaidi," alisema.

Shelukindo alisema mbali na msimu mpya wa vipindi hivyo, wateja wa DStv Poa wataendelea kufurahia vipindi vingine mbalimbali ikiwamo ile tamthilia maarufu ya Kapuni na Huba pamoja na vipindi vingine kemkem vya filamu, muziki na burudani.

"Tunaposema DStv Poa tunamaanisha bei Poa, ila yaliyomo humo ndani ni moto mkali! Na ndiyo maana tunasema 'Usichukulie Poa Vitu vya Poa' alisisitiza Shelukindo na kuwataka wateja wa DStv kuendelea kufurahia vipindi vyake na kutoa maoni yao ili yaweze kushughulikiwa.

## Ubalozi Ufaransa na Tamasha Hip hop Asili

**Na Faustine Feliciane**

UBALOZI wa Ufaransa nchini, umezindua msimu wa pili wa Tamasha la Muziki wa Hip Hop lililopewa jina la 'Tamasha la Hip Hop Asili', litakalofanyika kwenye viwanja vya Alliance de France kuanzia kesho mpaka Jumamosi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana katika ukumbi wa Kituo cha Utamaduni wa Ufaransa, Balozi wa nchi hiyo hapa nchini, Nabil Hajlaoui, alisema tamasha hilo litawakusanya vijana pamoja na kubadilishana ujuzi kupitia tamasha hilo.

Alisema Ufaransa inatambua ukubwa wa muziki huo ulioenea duniani kote, hivyo tamasha hilo litakusanya Waafrika katika mataifa mbalimbali kuadhimisha Hip Hop Asili chini ya balozi za nchi hiyo.

"Tamasha hili kwa mwaka huu pia tumeshirikiana na Ubalozi wa Marekani hapa Tanzania, tunaamini vijana kutoka mikoa mbalimbali waliopata nafasi ya kushiriki tamasha hili watapata fursa ya kuonyesha vipaji vyao na kukutana na vijana wenzako watakaobadilisha ujuzi na uzoefu kwenye muziki huo," alisema Balozi Hajlaoui.

Aidha, alisema tamasha hilo ni mwendelezo wa tamasha lililofanywa na baadhi ya wana Hip Hop 30 wa Afrika na Ufaransa Oktoba mwaka jana wakati wa mkutano wa 'New Africa-France Summit (NSAF)', ambao ulichochea kuandaliwa kwa mkakati wa ushirikiano wa Hip Hop kwa barani Afrika kwa kipindi cha 2022/2024.

Wasanii kutoka nchi za Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Kongo, Ghana, Mayotte, Ufaransa na Marekani wataungana na wasanii wengine 36 waliochaguliwa katika mashindano ya Hip Hop Asili kutoka mikoa sita ya Tanzania.

Mikoa hiyo ni Mwanza, Arusha, Mbeya, Dodoma, Dar es Salaam na Zanzibar.

Kwa upande wa Mkurugenzi wa Mipango wa Tamasha hilo, Matei Babu, alisema kwa kesho Hip Hop Asili litaandaa Shindano la kucheza kwa nchi za Afrika Mashariki ambapo Kwa Tanzania bingwa atakwenda kushiriki mashindano ya Dunia ya "Battle of the Year 2022" yatakayofanyika jijini Tokyo nchini Japan.

"Juni 25 tamasha litapambwa na wasanii wa Octopizzo (Kenya), Tina Mweni (Kenya/ Denmark), Rise up Band (Tanzania/Ufaransa), Jay Moe (Tanzania), The Mc 255 (Tanzania), Mic Crenshaw. (US), Lord Eyes (Tanzania) na wengine wengi," alisema Babu.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### LUKAKU SAFI INTER

KLABU ya Inter Milan ya Italia imekubali dili la kumsajili mshambuliaji Romelu Lukaku kwa mkopo wa msimu mzima kutoka Chelsea. 'The Blues' walimsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 kutoka Inter kwa pauni milioni 97.5 Agosti 2021, lakini atarejea katika kikosi hicho cha Serie A ambacho kilikuwa na matatizo msimu uliopita. (***Mail***)

### LEWANDOWSKI NA BAYERN

MSHAMBULIAJI wa Poland, Robert Lewandowski bado anataka kuondoka Bayern Munich, licha ya Mkurugenzi wa Michezo wa klabu hiyo ya Ujerumani, Hasan Salihamidzic kusafiri kukutana na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 ana kwa ana kujaribu kubadilisha mawazo yake. (***Sky Germany***)

### STERLING AWINDWA MADRID

REAL Madrid wameongeza nia ya kutaka kumnunua mshambuliaji wa England, Raheem Sterling katika wiki za hivi karibuni, huku Barcelona na Chelsea wakifuatilia maendeleo kuhusu mustakabali usio na uhakika wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, katika klabu ya Manchester City. (***Mirror***)

### EKITIKE AGOMBEWA ULAYA

REAL Madrid, Bayern Munich na Paris St-Germain ziko tayari kuchuana na Newcastle United kwa ajili ya kumsajili mshambuliaji wa Ufaransa, Hugo Ekitike mwenye umri wa miaka 20, kutoka Reims. (***L'Equipe***)

### KOUNDE ATAKIWA BARCA

BARCELONA wanataka kumsajili beki wa Ufaransa, Jules Kounde, lakini hawataki kulipa euro milioni 60 wanazotaka Sevilla kwa ajili ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23. (Marca)

### BRENTFORD YAMKOMALIA ERIKSEN

KLABU ya Brentford haijakata tamaa ya kumsajili mchezaji wa Denmark, Christian Eriksen, ambaye alijiunga nao kwa mkopo Januari kabla ya kuondoka mwishoni mwa msimu uliopita. Manchester United pia wanavutiwa na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30. (***90 Min***)

### ARSENAL KWA RUIZ

KLABU za Arsenal na Newcastle zinamtaka kiungo wa kati wa Hispania, Fabian Ruiz mwenye umri wa miaka 26, ambaye mkataba wake na Napoli utakamilika mwaka 2023. (***Corriere dello Sport, via Mail***)

### CLAUSS AMULIKWA CHELSEA

KLABU ya Chelsea wanavutiwa na beki wa pembeni wa Lens mwenye umri wa miaka 29, Jonathan Clauss. (***Goal***)

### HALLER KUTUA DORTMUND

KLABU ya Borussia Dortmund, ambayo ilimuuza mshambuliaji wa Norway, Erling Haaland mwenye umri wa miaka 21 kwa Manchester City, inatazamiwa kumsajili mshambuliaji wa Ivory Coast, Sebastien Haller kutoka Ajax kwa euro 36. (***ESPN***)

### WOLVES YASAKA NYOTA

KLABU ya Wolves inatarajiwa kufanya mazungumzo kuhusu kumsajili mshambuliaji wa Brazil, Gabriel Barbosa mwenye umri wa miaka 25, kutoka Flamengo na kiungo wa kati wa Argentina, Enzo Fernandez mwenye umri wa miaka 21, kutoka River Plate. (***90 Min***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# VINICIUS ATOA SABABU KUTAKA KUBAKI MADRID

●●● Nitaendelea katika timu kubwa zaidi duniani, ni timu iliyoungana tangu niwasili...

**MADRID,** Hispania

VINICIUS Junior ametangaza nia yake ya kusalia Real Madrid, akidai ndio timu "waliounganaʺ zaidi tangu alipowasili mwaka 2018.

Mbrazil huyo mwenye umri wa miaka 21, alifurahia mafanikio makubwa msimu huu uliopita, kwa kufunga mabao 17 na kusaidia 13 katika ushindi wa Real Madrid wa LaLiga, kabla ya kufunga katika fainali na kunyakua taji la 14 la Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Liverpool.

Amebakiza miaka miwili katika mkataba wake wa sasa, lakini anatarajiwa kurefusha hadi 2026, akikataa uvumi wa kutakiwa na Paris Saint-Germain.

**"Nitaendelea katika timu kubwa zaidi duniani," alisema akiiambia Sport TV. "Ni timu iliyoungana zaidi tangu niwasili. Sherehe zilikuwa tofauti mwaka huu. Sote tuli hisi kitu cha kipekee.**

"Watu wadogo walifika na mimi na Rodrygo, (Eder) Militao, (Eduardo) Camavinga. Kila mtu anapenda mwenzake na hilo ni muhimu.

"Ni mazingira bora zaidi duniani. Kila mtu anataka kuwa huko. Wenye uzoefu zaidi wanatupa amani ya akili na uhuru wa kufanya tunachotaka."

Wakati huo huo, Vinicius amekuwa mchezaji muhimu zaidi kwa timu ya Taifa ya Brazil, akicheza katika mechi saba kati ya 11 za mwisho za 'Selecao' hao za kufuzu Kombe la Dunia na kuanza tano kati ya hizo.

BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,008,5

MECHI KALI
KARLSLUNDS IF
VERSUS
IK GAUTHIOD
1 | 2.94
X | 3.77
2 | 2.03

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# RAIS PSG AMKATAA ZIDANE



**PARIS,** Ufaransa

RAIS wa Klabu ya Paris Saint Germain, Nasser Al-Khelaifi, amethibitisha kuwa klabu yake bado haijamfikiria Zinedine Zidane kuinoa klabu hiyo kwa sasa badala yake mikoba anaweza kupewa, Christophe Galtier.

Awali, kulikuwa na tetesi kuwa Zidane ndiye kocha aliyekuwa anapigiwa chapuo kuweza kuinoa klabu hiyo, huku ikisemekana kuwa Bodi ya PSG yote ilikuwa inaunga mkono azimio hilo, kabla ya Galtier kuingia kwenye kinyang'anyiro cha kuchukua mikoba ya Mauricio Pochettino.

"Tumefanya uchaguzi mwingine kuliko Zinedine Zidane. Tumemchagua kocha ambaye atakuwa bora kwetu kwa ajili ya kutuweka sehemu tunayostahili," alisema Al-Khelaifi akinukuliwa na vyombo vya habari vya Ufaransa.

"Mashabiki watakuwa wamevunjika moyo kumchagua Galtier dhidi ya Zidane? Ndoto yetu ni moja, ni uhalisia, kuwa na ndoto kubwa ni kitu kizuri lakini leo, inatupasa kuwa na uhalisia ukiachana na vyote."

Pia, alisisitiza kuwa Klabu ya PSG haikuwahi kufanya mazungumzo na Zidane kwa ajili ya kuinoa klabu hiyo.

# Tevez aanza kazi ya ukocha Argentina




**BUENOS AIRES,** Argentina

CARLOS Tevez amerejea katika soka kama kocha mkuu wa klabu ya Rosario Central ya nchini kwao, Argentina.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Manchester United, Manchester City na Juventus, ambaye alianza na kumaliza maisha yake ya uchezaji akiwa na Boca Juniors, alistaafu mapema Juni.

Uteuzi wake na Rosario Central ulithibitishwa Jumanne huku Tevez mwenye umri wa miaka 38, akikabidhiwa kazi yake ya kwanza ya ukocha na klabu hiyo kubwa.

Tevez alishinda mataji 26 katika maisha yake ya soka na ni miongoni mwa wachezaji wanne pekee wa Argentina walioshinda Copa Libertadores (Ligi ya Mabingwa Amerika Kusini), na kunyanyua tuzo kubwa zaidi katika soka kwa klabu barani Ulaya wakati alipobeba Ligi ya Mabin wa Ulaya akiwa na United mwal 2008.

Alikuwa mchezaji muhim wa timu ya Taifa ya Argentin kwa miaka mingi, akishirikian na Lionel Messi, Sergio Aguer na Gonzalo Higuain, lakini ak kosa kikosi cha Kombe la Dunia 2014, ambapo timu hiyo ilimaliz kama washindi wa pili nyuma y Ujerumani.

Mabingwa mara nne wa Arge tina, Rosario Central walifichu Jumanne kwamba Tevez amet saini mkataba wa mwaka mmoj na kutangaza kwenye Twitte "Apache anakuwa kocha mpy wa 'Dhahabu ya Bluu', baada y kusaini mkataba na klabu kw miezi 12."

Kabla ya Tevez kusaini mkatab wake, kipa Gaspar Servio aliiar bia TNT Sports: "Kwangu mim ni kitu maalum ambacho Carlit (Tevez) anaweza kuja hapa."

534,842/-

# KIKWETE MGENI RASMI SIMBA QUEENS VS FOUNTAIN GATE

**Na Shufaa Lyimo**

RAIS mstaafu wa Awamu ya Tatu, Jakaya Mrisho Kikwete, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika mechi ya kirafiki itakayozikutanisha Simba Queens dhidi ya timu ya Fountain Gate, ikiwa ni mchezo maalum kwa ajili ya kuadhimisha miaka 25 ya Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote (EOTF), imeelezwa.

**Akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana, Rais wa Shirikisho la Soka nchini, Wallace Karia, alisema wameungana na taasisi hiyo kuadhimisha wiki ya kusherehekea miaka 25 tangu mfuko huo ulipoanzishwa mwaka 1997.**

Alisema walitamani katika mchezo huo zikutanishwe Simba Queens na Yanga Princess, lakini walishindwa kuipata timu ya Yanga Princess kutokana na kuwa na udhuru.

"Imekuwa rahisi kuipata timu ya Simba Queens kwa kuwa wapo kambini wanajiandaa na michuano ya kimataifa," alisema Karia.

Rais huyo alisema ili kuuongezea nguvu mfuko huo, mwaka huu sehemu ya mapato yatakayopatikana kwenye mchezo wa Ngao ya Jamii watayapeleka mfuko wa taasisi hiyo.

Naye Mwenyekiti wa mfuko huo, Mama Ana Mkapa, alisema aliamua kuanzisha mfuko huo baada ya kuona kuna changamoto kwa akina mama, watoto pamoja na vijana kielimu na kiuchumi.

"Mfuko huu ulianzishwa mwaka 1997, niliamua kuanzisha baada ya kuona kina mama wengi wanapitia maisha magumu, hivyo nikaamua kutoa elimu ya afya, mpaka sasa tayari nimefanikiwa kuwapa elimu ya ujasiriamali kina mama 6,000 pamoja na vijana 1,755," alisema Mama Mkapa.

Alisema wameamua kushirikiana na TFF kwa kutambua michezo ni ajira na kwamba shirikisho hilo linaendesha shuhuli mbalimbali za michezo.

Kwa upande wa Msemaji wa TFF, Cliford Ndimbo, alisema mchezo huo utapigwa majira ya saa 9:30 alasiri huku ukitanguliwa na mechi ya ufunguzi itakayowakutanisha wake wa viongozi dhidi ya wanawake wajasiriamali.

Alisema mbali na mchezo huo pia kutakuwa na shughuli mbalimbali za kijamii ikiwamo zoezi la utoaji damu salama.

"Mchezo huo hautakuwa na kiingilio, tunawaomba Watanzania wajitokeze kwa wingi siku hiyo ili wajionee kazi zilizofanywa na mfuko huo," alisema Ndimbo.

## BONANZA...



Baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Awali ya Feza Zanzibar, wakishiriki michezo tofauti katika Bonanza maalum lililoandaliwa shuleni hapo kwa lengo la kuwajenga watoto kiafya ili baadaye kuwa fiti kushiriki mashindano tofauti ya michezo ndani na nje ya nchi **PICHA:MPIGAPICHA WETU**

# Singida Big Stars yakamilisha usajili asilimia 80

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa timu ya Singida Big Stars, umesema umekamilisha usajili wake kwa asilimia 80 ya wachezaji wapya kwa ajili ya kuimarisha kikosi chao kuelekea msimu ujao Ligi Kuu Tanzania Bara na michuano mingine.

Juzi Singida Big Stars ilimtambulisha mshambuliaji wa Mbeya Kwanza, Habib Kiyombo, na kueleza kuwa amesaini mkataba wa miaka miwili kuitumikia timu hiyo kuanzia msimu ujao.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Singida Big Stars, Hussein Massanza, alisema tayari wamefanya maboresho makubwa ndani ya kikosi cha timu hiyo ambayo yamekamilika kwa asilimia 80.

Alisema katika maboresho yaliyofanyika ni nafasi ya goli kipa, safu ya ulinzi na washambuliaji ambao wataenda kumuongezea nguvu Amissi Tambwe ambaye anaendelea kuitumikia timu hiyo.

"Tunaendelea kuimarisha kikosi cha timu yetu na tumeshafanya usajili kwa asilimia 80, sehemu iliyobaki ni ndogo ikiwamo kuboresha benchi la ufundi kuwa imara," alisema Massanza.

Alisema katika nafasi iliyobaki ni sehemu ya benchi la ufundi ikiwamo kupatikana kwa kocha mpya ambaye atakinoa kikosi cha timu hiyo kwa msimu ujao.

Alisema mikakati yao mikubwa ni kuanza maandalizi mapema ikiwamo timu hiyo kuingia kambini Julai 15 au 20, mwaka huu wakianza kambi hiyo jijini Dar es Salaam.

Hata hivyo, licha ya kufanya siri kuhusu usajili wao, Nipashe limepata taarifa kuwa tayari timu hiyo imemalizana na kipa wa Polisi Tanzania, Metacha Mnata, beki wa KMC FC, Andrew Vicent 'Dante' na Abdul- Majid Mangalo kutoka Biashara United.

Wengine ni beki wa Simba, Michael Gadiel, Aziz Andambwile kiungo kutoka Mbeya City na beki wa Yanga, Paul Godfrey 'Boxer'.


## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 25/06/22 | 22:10 | Club Atletico Alvarado vs Belgrano | 3.50 | 2.90 | 2.33 |
| 02. 25/06/22 | 22:30 | Atletico PR vs Bragantino SP | 2.44 | 3.03 | 3.08 |
| 03. 26/06/22 | 00:00 | DC United vs Nashville | 2.43 | 3.40 | 2.85 |
| 04. 26/06/22 | 00:00 | Colon Santa Fe vs Huracan | 2.35 | 3.28 | 3.13 |
| 05. 26/06/22 | 02:30 | Toronto vs Atlanta United | 2.96 | 3.51 | 2.32 |
| 06. 26/06/22 | 05:00 | San Jose Earthquake vs Los Angeles Galaxy | 2.61 | 3.56 | 2.56 |
| 07. 26/06/22 | 05:30 | Portland Timbers vs Colorado Rapids | 2.26 | 3.43 | 3.12 |
| 08. 26/06/22 | 12:00 | Vissel Kobe vs Urawa Red Diamonds | 2.78 | 3.23 | 2.63 |
| 09. 26/06/22 | 12:00 | Nagoya Grampus vs Kashima Antlers | 2.92 | 3.28 | 2.48 |
| 10. 26/06/22 | 12:00 | Yokohama vs Niigata Albirex | 2.59 | 3.24 | 2.74 |
| 11. 26/06/22 | 12:30 | Kyoto Sanga vs Shonan Bellmare | 2.73 | 3.29 | 2.63 |
| 12. 26/06/22 | 13:00 | Omiya Ardija vs Zwiegen Kanazawa | 2.91 | 3.21 | 2.48 |
| 13. 26/06/22 | 19:00 | Ham-Kam vs Sarpsborg | 2.74 | 3.43 | 2.45 |
| 14. 26/06/22 | 19:00 | Sandefjord vs Tromso | 2.78 | 3.42 | 2.42 |
| 15. 26/06/22 | 19:00 | Stromsgodset vs Lillestrom | 2.73 | 3.42 | 2.46 |
| 16. 26/06/22 | 19:00 | San Lorenzo vs Tigre | 2.84 | 3.30 | 2.54 |
| 17. 26/06/22 | 22:00 | Botafogo RJ vs Fluminense | 2.52 | 3.12 | 2.87 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### ALHAMISI - 23/06/2022

| MUDAVV | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:45 | 2654 | Huracan Reserve vs Colon de Santa Fe Reserve | 2.10 | 3.13 | 3.28 |
| 16:00 | 2733 | Addis Ababa City FC vs Sebeta City FC | 2.38 | 2.85 | 3.25 |
| 17:00 | 3781 | CA Union Santa Fe Reserve vs Boca Jrs | 4.31 | 3.68 | 1.68 |
| 17:00 | 4607 | Kedainiai Nevezis vs FA Siauliai B | 1.67 | 3.77 | 4.21 |
| 17:30 | 1761 | Gasovik Vitebsk vs Dnepr Mogilev | 12.00 | 7.40 | 1.16 |
| 18:00 | 1592 | Qizilqum vs Pakhtakor | 5.69 | 3.48 | 1.57 |
| 18:00 | 3008 | Lida vs FK Arsenal Dzerzhinsk | 11.78 | 6.28 | 1.17 |
| 18:00 | 4660 | Jippo vs Nurmijarven Jalkapalloseura | 1.38 | 4.81 | 5.89 |
| 18:00 | 5504 | FK Atmosphere vs FK Vilnus Bfa | 2.41 | 3.60 | 2.60 |
| 18:30 | 1395 | Naftan Novopolotsk vs FC Minsk | 6.40 | 4.30 | 1.45 |
| 18:30 | 1555 | Kerho 07 vs Pepo Lappeenranta | 1.78 | 3.64 | 3.79 |
| 18:30 | 3005 | FC Honka/Akatemia vs Vjs | 1.66 | 4.02 | 4.02 |
| 18:30 | 3212 | JBK Pietarsaari vs Narpes Kraft | 1.85 | 3.79 | 3.39 |
| 18:30 | 3512 | Klubi 04 vs EPS | 1.36 | 4.52 | 7.07 |
| 18:30 | 3939 | FC Futura vs Lahden Reipas | 3.84 | 4.24 | 1.66 |
| 18:30 | 4004 | JJK Jyvaskyla vs JS Hercules | 1.49 | 4.31 | 5.09 |
| 18:30 | 4565 | Ilves 2 vs Kaapo Kaarina | 1.64 | 4.13 | 4.03 |
| 19:00 | 2473 | IFK Ostersund vs Bergnasets Aik | 1.27 | 5.51 | 7.67 |
| 19:00 | 3387 | Bodens BK vs Kiruna FF | 1.18 | 6.33 | 10.88 |
| 19:30 | 4711 | Husqvarna FF vs Tolo IF | 1.06 | 9.63 | 18.66 |
| 20:00 | 1634 | Ahlafors IF vs Nordvarmland FF | 1.32 | 4.92 | 7.27 |
| 20:00 | 2138 | Friska Viljor FC vs Gottne IF | 1.71 | 4.02 | 3.77 |
| 20:00 | 2694 | Nosaby IF vs Kristianstads FF | 3.15 | 3.90 | 1.97 |
| 20:00 | 3108 | Hogsby IK vs IFK Berga | 3.75 | 3.75 | 1.82 |
| 20:00 | 3649 | FBK Balkan vs Osterlen FF | 4.20 | 4.10 | 1.68 |
| 20:00 | 3827 | Skiljebo SK vs IFK Uppsala | 1.46 | 4.52 | 5.11 |
| 20:00 | 3870 | Hittarps IK vs Hoganas BK | 1.19 | 7.00 | 10.00 |
| 20:00 | 3937 | Gefle IF vs IFK Haninge | 1.79 | 3.79 | 3.59 |
| 20:00 | 4485 | Hammarby Talang FF vs IF Sylvia | 2.75 | 3.70 | 2.26 |
| 20:00 | 5219 | IFK Hassleholm vs Eslovs BK | 1.60 | 4.10 | 4.70 |
| 20:00 | 5309 | BK Forward vs Vasalunds IF | 6.00 | 4.50 | 1.45 |
| 20:00 | 5662 | FK Karlskrona vs Hassleholms IF | 3.75 | 3.75 | 1.82 |
| 20:30 | 1177 | Karlslunds IF vs IK Gauthiod | 2.94 | 3.77 | 2.03 |
| 20:30 | 1344 | Assyriska BK vs Eskilsminne IF | 19.00 | 9.60 | 1.08 |
| 20:30 | 1614 | IFK Luleaa vs Storfors Aik | 1.29 | 5.10 | 7.64 |
| 20:30 | 1906 | Enskede IK vs IFK Eskilstuna | 1.29 | 5.60 | 8.00 |
| 20:30 | 3800 | Herrestads AIF vs Saffle FF | 2.55 | 3.77 | 2.26 |
| 20:30 | 4520 | Ullareds IK vs Varbergs Gif FK | 2.21 | 3.85 | 2.70 |
| 21:00 | 2520 | Huddinge IF vs Syrianska | 2.76 | 3.60 | 2.18 |
| 21:00 | 3702 | Vikingur Gota II vs IF Fuglafjordur | 2.65 | 3.80 | 2.26 |
| 21:00 | 4408 | Belgium W vs Northern Ireland W | 1.20 | 5.47 | 11.73 |
| 21:15 | 4578 | IFK Kumla vs Vanersborgs FK | 2.28 | 3.80 | 2.51 |
| 22:15 | 3324 | Grotta vs Fylkir | 2.76 | 3.60 | 2.18 |
| 22:15 | 4025 | Breidablik vs KR Reykjavik | 1.68 | 3.83 | 4.12 |
| 22:15 | 4977 | HK Kopavogs vs Kordrengir | 1.95 | 3.63 | 3.19 |

### IJUMAA - 24/06/2022

| MUDAVV | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01:00 | 1930 | Fluminense vs Cruzeiro | 1.78 | 3.27 | 4.30 |
| 01:00 | 2212 | Deportes Temuco vs Colo Colo | 5.52 | 3.84 | 1.52 |
| 03:30 | 2335 | Ponte Preta vs Sampaio MA | 2.06 | 3.14 | 3.38 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Alhamisi Juni 23, 2022
Nipashe




**Vinicius atoa sababu kutaka kubaki Madrid**

RASMI...




Mshambuliaji wa Liverpool, Msenegal Sadio Mane, amejiunga rasmi na Bayern Munich. **PICHA: MTANDAO**

## Dirisha la usajili wazi Julai Mosi

**Na Adam Fungamwango**

DIRISHA la usajili wa wachezaji kwa ajili ya Ligi Kuu Tanzania Bara, Ligi ya Championship, Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara na Ligi ya Wanawake msimu wa 2022/23, linatarajiwa kuanza rasmi Julai Mosi na kumalizika Agosti 31, mwaka huu.

Taarifa iliyotolewa na Shirikisho la Soka nchini (TFF), jana ikisainiwa na Ofisa Habari na Mawasiliano wake, Cliford Ndimbo, imetahadharisha kuwa hakutakuwa na muda wa ziada baada ya dirisha hilo kufungwa.

"Dirisha la Usajili kwa klabu za Ligi Kuu, Championship, 'First League', na Ligi Kuu ya Wanawake msimu wa 2022/23 litafunguliwa Julai Mosi na kufungwa Agosti 31, mwaka huu.

"Katika kipindi hicho klabu zinatakiwa kukamilisha usajili na uhamisho wa kimataifa. Klabu zote zinapaswa kuzingatia muda huo wa usajili, hakutakuwa na muda wa ziada baada ya dirisha kufungwa. Yeyote atakayekutana na changamoto awasiliane na Idara ya Mashindano TFF.

"Aidha dirisha dogo, lenyewe litafunguliwa Desemba 16, mwaka huu na kufungwa Januari 15, 2023," ilihitimisha taarifa hiyo.

# Sherehe ya Kombe Yanga 'babkubwa'

**Ubwabwa kuliwa, Bodi ya Ligi yapitisha sherehe kuanzia Mbeya hadi Dar, wenyewe wasema litapita Msimbazi kwanza...**

**Shufaa Lyimo na Adam Fungamwango**

WAKATI Bodi ya Ligi nchini (TPLB), ikiweka wazi kuwa mabingwa wapya wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga, watakabidhiwa kombe lao Jumamosi kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya baada ya mechi yao dhidi ya Mbeya City, uongozi wa klabu hiyo umetangaza dhamira yao ya kufanya sherehe 'babkubwa' kusherehekea taji hilo.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Habari wa Bodi ya Ligi Tanzania, Karim Boimanda alisema maandalizi ya kuelekea sherehe hizo za ubingwa yanaendelea vizuri na kwamba itautumia mchezo huo namba 225 wa mzunguko wa 29 kukabidhi kombe la ubingwa wa ligi msimu wa 2021/22.

Alisema tayari maofisa wa mchezo huo wamejulishwa uwapo wa tukio na maandalizi hayo.

Hata hivyo, haitokuwa mechi ya mwisho kwa timu hiyo, kwani itamaliza msimu Juni 29, mwaka huu itakapocheza dhidi ya Mtibwa Sugar kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

"Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), inatangaza kuutumia mchezo namba 225 wa mzunguko wa 29 wa ligi kati ya Mbeya City dhidi ya Yanga kukabidhi kombe la ubingwa wa ligi msimu wa 2021/22.

"Mabingwa wapya wa Ligi Kuu Klabu ya Yanga ya Dar es Salaam, watakabidhiwa kombe lao katika sherehe zitakazofanyika baada ya kumalizika kwa mchezo huo uliopangwa kuchezwa Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini Mbeya Juni 25. Wadau na maofisa wa mchezo huo wamejulishwa juu ya uwapo wa tukio hilo na maandalizi yanaendelea vema," alisema.

Aidha, Bodi ya Ligi imesema inawakaribisha wadau wote kwenye tukio hilo la kuhitimisha msimu wa 2021/22.

Kwa upande wa uongozi wa Yanga, Msemaji wa klabu hiyo, Haji Manara, amesema watafanya sherehe kubwa kuanzia Mbeya baada ya kukabidhiwa kombe hilo hadi Dar es Salaam.

Akizungumza Dar es Salaam jana, Manara alisema sherehe hizo zitaanzia Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine na kuendelea jijini Mbeya kabla ya 'mwali' wao huyo kupandishwa ndege kuelekea Dar es Salaam kwa sherehe zaidi.

"Tumeandaa basi maalum la kifahari ambalo linatarajiwa kutua siku yoyote kuanzia leo, kama wanavyofanya Real Madrid, Chelsea na Liverpool, sisi hatuwezi kupandisha kombe kwenye Fusso," alisema.

Manara alisema baada ya kutua Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere, Dar es Salaam, chereko chereko zitaanzia hapo kuelekea Makao Makuu ya klabu hiyo, mtaa wa Twiga na Jangwani ambapo zitapitia mtaa wa Msimbazi.

Alisema baada ya kufika makao makuu ya klabu hiyo, dua maalum ya kumshukuru Mungu kwa kuwawezesha kutwaa taji hilo itasomwa ikifuatiwa na 'ubwabwa' kwa mashabiki na wanachama wa klabu hiyo.

Alisema baada ya hapo wataelekea ufukweni, Kidimbwi ambapo mashabiki na wanachama watapata fursa ya kupiga picha na kombe hilo katika sherehe hizo.

Yanga imetwaa ubingwa kwa mara ya kwanza baada ya misimu minne ambayo yote ilikuwa inachukuliwa na timu ya Simba.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >